ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais

20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu

53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thelathini na Moja - Tarehe 20 Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha Baraza cha tarehe 2 Juni, 2017, Mhe. Mohamed Said Mohamed aliuliza swali la nyongeza kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, wizara hiyo imeleta majibu kama waziri wa wizara hiyo alivyoahidi.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa namuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora asome jibu la swali la nyongeza aliloulizwa na Mhe. Mjumbe huyo.

Waheshimiwa Wajumbe, aidha, katika kikao cha Baraza cha tarehe 7 Juni, 2017, Mhe. Maryam Thani Juma aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Sasa namuomba Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi asome jibu la swali la nyongeza aliloulizwa na Mhe. Mjumbe huyo. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninajibu swali Namba 187, niliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Mohamed Said Mohamed aliyetaka kujua ni nyaraka ngapi ambazo zilizokwisha kufanyiwa kazi kutoka katika mfumo wa "*manual*" kwenda katika mfumo wa kielektroniki na je, vifaa hivyo vimegharimu kiasi gani mpaka kufikia katika sehemu husika.

Mhe. Mwenyekiti, Idadi ya Nyaraka ambazo zimekwisha fanyiwa kazi kutoka mfumo wa karatasi kwenda mfumo wa kielektroniki ni nyaraka 74 ambazo zina *folio* 9,488.

Mhe. Mwenyekiti, vifaa hivyo vimegharimu jumla ya shilingi 249,994,140. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi akijibu swali la nyongeza namba 14, lililoulizwa na Mhe. Maryam Thani Juma, ambaye alitaka kujua ni kiasi gani cha fedha kilichopatikana baada ya ukodishwaji wa mashamba ya mikarafuu kwa mwaka wa 2016 na 2017.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali hilo la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, fedha zilizopatikana baada ya ukodishwaji wa mashamba hayo kwa mwaka 2016 ni shs. 30,158,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

WILAYA	FEDHA ZILIZOPATIKANA
MKOANI	21,719,000
CHAKE CHAKE	3,132,000
WETE	5,307,000
JUMLA	**30,158,000**

Mhe. Mwenyekiti, Wilaya ya Micheweni hakukuwa na uzazi kwa msimu huo wa karafuu. Kwa mwaka wa 2017, ukodishwaji wa Mikarafuu unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi wa Juni, 2017 kwa msimu wa mwaka huu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hati juu ya Hotuba ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Trilioni Moja Bilioni Thamanini na Saba Milioni Mia Tatu Hamsini na Tisa na Laki Nne kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia siku ya tarehe Thelathini Juni, mwaka Elfu Mbili na Kumi na Nane na Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Endelea tena Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (**Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti):** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Katibu kwa shughuli inayofuata.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 96

Utaratibu wa Kurejeshewa Mifugo Iliyokamatwa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na zoezi la kukamata mifugo inayodaiwa kufungwa kinyume na taratibu za usafi wa miji. Hata hivyo, baadhi ya wananchi wamekuwa hawafahamu njia na taratibu za kupita ili kurejeshewa mifugo yao.

Je, ni utaratibu gani wananchi ambao mifugo yao imekamatwa wanatakiwa wapite ili warejeshewe mifugo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 96 naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, chimbuko la uondoaji wa wanyama katika maeneo ya mji ni agizo la serikali lilitolewa tokea mwaka 2010, mara baada ya Serikali ya Awamu ya Saba kuingia madarakani. Agizo hilo lililenga kuimarisha usafi wa mji, usalama barabarani na kuweka mandhari nzuri na yenye kuvutia kwa kupendeza ndani ya mji wetu kama ilivyo miji mengine duniani.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia kutolewa kwa agizo hilo pamoja na malengo mazuri ya zoezi hilo kwa mustakbali wa nchi na wananchi wake, serikali kupitia Mkoa wa Mjini/Magharibi iliandaa utaratibu kwa kuzingatia misingi ya kisheria na kuweka miongozo thabiti ya kutekeleza agizo hilo ikiwemo kuwaita wafugaji, masheha na baadhi ya wananchi kupitia Serikali za Mitaa ili kuwapa elimu na uelewa wa kutosha wahusika wote juu ya jambo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa azma hii njema ya serikali kwa wananchi wake mnamo mwezi Mei mwaka 2016, Serikali ya Mkoa wa Mjini/Magharibi ilitoa maelezo zaidi ya ufafanuzi na muongozo pamoja na kuwapa muda wa wiki moja wananchi kuondoa mifugo yao katika maeneo yaliyokatazwa kutunzwa au kuzurura. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana wapo baadhi

ya wananchi hawakutekeleza vyema agizo hilo la serikali na kupelekea serikali kuchukua hatua za kisheria mara baada ya muda uliotolewa kumalizika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo sasa kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake namba 96 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wanyama wote waliokamatwa na watakaokamatwa wanatunzwa katika eneo maalum liliopo miongoni mwa maeneo ya kambi za vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambako wanyama hao huhifadhiwa pamoja na kupewa matunzo yote yanayostahiki ikiwemo chakula na maji. Utaratibu wa kuwapata tena wanyama hao ni kuchukua barua katika Shehia anayofugwa mnyama husika na kuiwasilisha barua hiyo kwa utambuzi katika Manispaa yake.

Mhe. Mwenyekiti, mfugaji atafafanuliwa gharama za ufugaji katika eneo lisilokubaliwa na atatakiwa kulipa gharama za utunzaji wa wanyama hao kwa kipindi chote alichokaa mnyama huyo katika hifadhi ya serikali na hatimae anakabidhiwa mnyama wake akiwa amewekwa alama maalum kwa lengo la udhibiti wa kurudia tena kuwaweka wanyama hao katika maeneo yasiyoruhusiwa kufugwa. Endapo mnyama aliyewekwa alama atakamatwa tena katika maeneo hayo hayo yasiyoruhusiwa, basi mnyama huyo atakuwa mali ya serikali na taratibu husika za kuuzwa zitafuatwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa mara ya kwanza kujibu swali kwa kikamilifu swali la msingi. Mhe. Naibu Waziri hongera sana, kwa mara yangu ya mwanzo kukuuliza swali la msingi ukajibu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri huoni kuwa serikali imepitikiwa au mmesahau na sio aibu kukamata mifugo ile mwanzo na wakati sheria ilikuwa haipo na sisi wajumbe humu sote ni mashahidi, baada ya kukamata mifugo ile ndio tukaleta sheria na Mwenyezi Mungu anatusikia Ramadhani hii, sio aibu na Mhe. Waziri hilo analijua alikutana pia na wanasheria wake akawaambia kuna sheria ipi, tukafika pahali tukakwama. *(Makofi)*

Je, huu mwezi Mtukufu wa Ramadhani tumekusudia Waziri wetu wa Fedha na Mipango kwa umakini wake wa hali ya juu alitoa msamaha kwa wananchi wake, kama mchele, sukari, tende na unga wa ngano. Serikali ndio wananchi na wananchi ndio serikali, bila ya kuwepo serikali wananchi wasingekuwepo na wananchi ndio serikali. Hamuoni kutoa msamaha katika mwezi mtukufu mkawasamehe na ikawa fundisho kwa wengine. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili, Je tangu utaratibu huu wa kukamata ng'ombe, ni ng'ombe wangapi mmewakamata na wangapi wamekombolewa, na wale waliozaa yale maziwa yanakwenda wapi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba Mhe. Mwakilishi alirudie swali lake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba urejee swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, swali lipi, la mwanzo au la pili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba arejee yote.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, rejea yote mawili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haya ngoja nizungumze kidogo kidogo Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri haoni kama serikali tuseme imesahau au imepitikiwa kukamata mifugo ile wakati sheria mlikuwa hamna, na sisi wajumbe sote humu ni shahidi, baada ya kukamata mifugo na kelele zetu Waheshimiwa Wawakilishi, ndipo ikaja sheria humu ndani na huu mwezi Mtukufu wa Ramadhani nazungumza maneno hayo. Sio aibu na kuteleza sio kuanguka.

Mhe. Waziri hili analijua. Mwenyewe alikutana na wanasheria wake anapajua wapi alipokutana nao akawauliza. Akaambiwa sheria huna Mhe. Waziri, ndio baadae ikaja sheria humu ndani. Nasema tena serikali mnapokuwa mkijibu humu ndani hamuogopi hasara kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub uliza maswali mawili ambayo unataka kuuliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tumeshuhudia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango juzi katoa msamaha kwa wannachi wake ikiwemo sukari, unga wa ngano, mchele na tende.

(a) Je, hamuoni hivi sasa wakati umefika na nyinyi angalau tukawafurahisha wananchi wetu katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani ili msamaha huu ukatoka. Tukumbuke kuwe serikali ndio wananchi na wananchi ndio serikali That is (a).

(b) Je, tangu uanze utaratibu wa mifugo ni mifugo mingapi mliyokamata na mifugo mingapi watu wamelipa gharama zao na kuikomboa mifugo hiyo, na ni maeneo gani. Maana yake kuna maeneo mengine ng'ombe kakata njia tu kakamatwa kakata kamba kufukuzia mlo.

Vile vile kuna mifugo mingine imezaa ndani je, yale maziwa yanakwenda wapi?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niyajibu maswali ya nyongeza ya Mhe. Mwakilishi ambayo yamezidi, lakini nitaendelea kuyajibu yote.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe kusema kwamba serikali imepitikiwa. Naomba nijibu kwamba serikali haijapitikiwa, ilifanya maamuzi haya kwa umakini na maagizo haya yalizingatia yale yote ambayo yalikuwa ni kero kwa wananchi kama vile ambavyo labda ilionekana ni kero.

Lakini sambamba na hilo Mhe. Mwenyekiti, kuhusu sheria kwamba ilikuwa bado haijakuwepo. Naomba nimkumbushe Mhe. Mwakilishi sheria namba 3 ya mwaka 2015 ya mazingira, hii ni moja katika ambayo imetumika katika kulitekeleza agizo hili. Lakini vile vile tukumbuke kwamba suala la misamaha. Mhe. Mwakilishi mimi nikuombe sana pamoja na waheshimiwa wengine, kwamba tatizo hili ni kwamba limekuwa endelevu na hivi ninavyokuambia bado

baadhi ya wananchi wengine tunapata taarifa zisizorasmi kwamba bado mifugo wanaiingiza kinyemela.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo niseme kwamba suala la msamaha kwa hili, naomba Waheshimiwa Wajumbe mtusaidie katika kuwasaidia wananchi kuwaelimisha umuhimu wa jambo hili na sio kusimama tukajaribu kuwakingia kifua, kwa sababu sheria hizi ambazo tumezitumia sisi ni kwamba tumezipitisha katika chombo hiki kitukufu ambacho ndio tegemeo katika kupitisha na kutunga sheria za nchi yetu. Kwa hivyo, ni vyema Waheshimiwa Wajumbe, basi tuwasaidie wananchi kuwahamasisha kufuata sheria bila ya kushurutishwa. Lakini kwa hili niseme tu Mhe. Mjumbe msamaha huu hapana na zoezi hili litakuwa ni endelevu mpaka pale hali itakapokuwa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu jumla ya wanyama ambao wamekamatwa tokea zoezi hili kuanza. Nimwambie kwamba kuanzia Julai, 2016 mpaka Mei, 2017 ni jumla ya wanyama 222 wamekamatwa na kati yao kuna ng'ombe 121 na vile vile kuna mbuzi 78 na kuna punda wapatao 23.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la maziwa kwamba kunazalishwa maziwa na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, hili hadi sasa hivi hatujapata taarifa kwamba kuna maziwa yanayopatikana. Lakini tukumbuke kwamba zile fedha zinazopatikana kwa kadhia hii, kwa sababu sisi hatufanyi kama ni chanzo cha mapato hiki, zinatumika katika kuwahudumia mifugo hii hii ambayo imekamatwa tukizingatia kwamba mifugo ile inahitaji malisho na hususan kipindi cha kiangazi tulichotoka. Lakini vile vile kuna madawa na maji na huduma nyengine.

Kwa hivyo, kiufupi hatuna makusanyo ambayo tunayapata kwa kupitia maziwa ama jambo jengine kwa kupitia wanyama ambao wamekamatwa.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala dogo la nyongeza. Kwanza nipongeze juhudi za Serikali za kudumisha usafi katika miji yetu.

a) Mhe. Waziri, inaonekana Miji Pemba hakuna na hakuna kwasababu ni kitu gani kinasababisha mifugo Pemba isikamatwe ndani ya miji.
b) Je, hamuoni kwamba mnada wa ng'ombe katika mji wa Chake Chake upo ndani ya mji na mmeuweke nyinyi, na kuuweka mnada ule ndani ya Mji hamuoni kama mnasababisha uchafu wa mji ule, na huyo aliyeweka hatua ya kuweka mnada hamuoni kwamba kapuuza agizo na sheria hii mliyoweka ya kusafisha miji yetu na hatua gani mtamchukulia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwanyekiti, naomba niendelee kumjibu Mhe. Mjumbe mahiri sana kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, itakumbukwa katika kipindi cha bajeti tuliweza kutoa ufafanuzi juu ya jambo hili kwamba agizo hili lilihusu miji yote ikimaanisha pia Chakechake, Wete na Mkoani kwa kisiwa cha Pemba, na wakati nilipokuwa najibu katika kutoa ufafanuzi baadhi ya majibu

tulisema kwamba hili ni agizo la Serikali na kama agizo la Serikali linatakiwa litumike katika maeneo yote ambayo agizo hili limetoka.

Sasa kwakuwa Mhe. Mjumbe amesema mnada wa ng'ombe upo ndani ya Chakechake nimwambie kwamba kweli kama hilo zoezi linaendelea ni uchafu na tumeshatoa maagizo naomba tutachukua hatua kuona kwamba tunatafuta namna bora ya kuona kwamba Mji wa Chakechake nao unakuwa salama katika kuepukana na madhara haya ambayo yanatokana na mifugo. Kwahivyo, naomba Mhe. Mjumbe anipe muda tukimaliza Baraza tutaangalia utaratibu uliopo mzuri na tutashirikiana na wewe kutafuta saiti bora ambayo itatusaidia katika kukabiliana na hali hii.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza suala la nyongeza, kwanza nampongeza sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub Muwakilishi wa Jimbo la Paje kwa suala lake zuri sana linaogusa maisha ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kama suala la msingi alivyouliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba hawa wanyama walivyokamatwa walikamatwa utaratibu yale marekebisho ya kanuni hazijafanywa, sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa utaratibu sheria zote ambazo tunazozitunga inatakiwa inaana kutumika tarehe ile mara baada ya kutumika.

a) Je, hatuoni suala la Mhe. Jaku ni kwamba iko haja ya wale wanyama ambao walikamatwa kabla hizi sheria kufanyiwa marekebisho warejeshewe wenyewe.

b) Mhe. Mwenyekiti, serikali ina majukumu mengi leo kuwacha shughuli zote ambazo tunazozipitisha hapa Barazani wakenda kukaa kuwashughulikia wanyama ambao wananchi wenyewe walikuwa hawajashindwa kuwahudumia je, hatuoni kwamba serikali kujibebesha mizigo iliyokuwa haina maana.

c) Mhe. Mwenyekiti, kama alivyouliza Mhe. Hamad Abdalla Rashid kwamba kwakuwa Unguja tayari kuna ile sheria na utaratibu wa kuweza kuwakamata wanyama mjini, kwa nini sheria hii haifanyi kazi mpaka Pemba, au kuna sheria sasa hivi tunazozitunga kwamba zinatumika upande mmoja tu Unguja Pemba hazitumiki, au Sheria inatumika Pemba Unguja haitumiki.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekuona Mhe. Waziri kwa majibu lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu jibu suala (a) na (b).

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake nye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Kwanza nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu mazuri sana ambayo ameyatoa tokea wakati wa kujibu hoja, wakati wa kujadili bajeti ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ Mhe. Naibu Waziri hongera sana na unafaa kuvaa kiatu changu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kama alivyosema Mhe, Naibu Waziri kwenye jibu lake mama kwamba sheria zipo na *Local Government* kwa maana ya mabaraza ya Miji, Mabaraza ya Manispaa, Halmashauri yanafanyakazi sheria ambazo zilikuwepo zamani kabla ya kuwepo kwa Sheria No. 7 ya mwaka 2014. Waheshimiwa Wajumbe waelewe kwamba zilikuwepo sheria zilikuwepo kanuni lakini pia Mhe. Naibu Waziri amesema tulifanyia kazi sheria ya mazingira na sheria ya uzururaji wa wanyama hizo sheria zote zipo na zimepitishwa na Baraza hili tukufu.

Kwa hivyo si kweli kabisa kwamba tumetekeleza halafu ndipo tukaja tukatunga sheria kilichofanyika ni kwamba baada ya sheria No. 7 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014 tumeitengenezea kanuni, hizo kanuni ambazo tumezitunga zimeweka nguvu zaidi za utekelezaji na usimamizi kuliko zile kanuni ambazo zilikuwepo hapo awali. Kwa hivyo naomba nichukue fursa hii kusema kwamba tumefanya kazi kwa kutumia sheria, lakini vile vile tumefanyakazi vile vile kwa kupata au kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Baraza hili hili ndilo ambalo lilikuwa linatuhimiza kwamba kauli za kimapinduzi hazibezwi lazima zifanyiwe kazi.

Lakini kuhusu suala la sheria hii kufanya kazi sehemu moja tu ya Zanzibar, sheria yoyote inayotungwa ndani ya Baraza hili inatakiwa ifanye kazi nchi nzima, sasa kama kuna kasoro ya utekelezaji au ya usimamizi wa sheria hii upande wa pili wa Zanzibar kwa maana kisiwani Pemba, kama aivyosema Mhe. Naibu Waziri tulishatoa maelekezo na baada tu ya kumaliza mkutano huu wa bajeti basi tutachukua hatua na maeneo mengine yoyote ya Zanzibar ili kuhakikisha sheria tunazozipitisha hapa zinafuatwa na tunakwenda bila ya kumuonea mtu. Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Nam. 24

Marekebisho ya Sheria ya Ukatili wa Kijinsia

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:

Sheria inayohusiana na Ukatili wa Kijinsia haiendani na wakati uliopo hivi sasa na hivyo kusababisha vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto kuzidi katika jamii.

Je, ni lini Sheria hii itafanyiwa Marekebisho ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba jamii yetu kama ilivyo kwa jamii nyengine Duniani, imekumbwa na tatizo kubwa linalohusiana na ukatili wa kijinsia

hususani kwa wanawake na watoto. Aidha Serikali kupitia taasisi zake na kwa kushirikiana na Asasi za kiraia imekuwa ikichukua hatua mbali mbali kukabiliana na tatizo hili.

Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya hatua za kuchukua iwapo udhalilishaji utatokea, jinsi ya kuepuka udhalilishaji huo, wazazi na walezi kufuatilia nyendo za watoto wetu na hatua nyengine zinazolenga kukabiliana na vitendo hivi.

Mhe. Mwenyekiti, masuala yanayohusiana na ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto na hatua za kuchukulia iwapo matendo hayo yatatokea yameelezwa vizuri katika Sheria ya Mwenendo wa Adhabu Namba 6 ya 2004 na Sheria ya Mwenendo wa Jinai Namba 7 ya 2004. Sheria zote hizi zimo katika hatua za mwisho za kufanyiwa mapitio ili hatimae ziwasilishwe katika kikao cha Baraza la Wawakilishi ili Waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mpate nafasi ya kuzipitia na kutoa maoni yenu na hatimae kuzipitisha.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza suali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Waziri Je marekebisho uliyoyafanya katika sheria hizo yamezingatia kuweka adhabu ya mtoto anayemdhalilisha mtoto mwenzake kijinsia.

(b) Ni lini Mhe. Waziri sheria hizo zitawasilishwa Barazani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hizi zote mbili ambazo zinahusiana namasuala ya udhalilishaji zimekidhi haja kwa maana ya kwamba hazijaacha kitu chochote, kwa hivyo Mheshimiwa asiwe na wasi wasi na hilo kwa maana kwamba sheria hizi zimekidhi haja zote ili udhalilishaji uweze kukomeshwa Zanzibar.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, suala (b) ni lini nimwambie tu Mhe. Muwakilishi kwamba tunategema mwaka wa fedha ujao sheria hizi zitaletwa barazani ahsante.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza suali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa amekiri kwamba sheria hizi zina kuondosha kabisa tatizo hili la udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mheshimu Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, marekebishao ya sheria zote hizi mbili ni kwamba yamesheheni mambo mengi mambo ambayo mazuri, mambo ambayo hata yakiletwa katika Baraza hili la Wawakilishi

naamini kwamba Wajumbe mtafurahia na mtaweza kuyachangia ili kufikia lile lengo la kwamba udhalilishaji uweze kutokomezwa hapa Zanzibar.

Lakini nije moja kwa moja katika suali lake ni kwamba mambo gani ambayo Serikali imeyaona ni muhimu kuyafanyia marekebisho baada ya kupata maoni sehemu mbali mbali, kwanza mwanzo na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi ni mashahidi wa hayo kulikuwa waheshimiwa wengi wanazungumza suala la Mahakama za chini kwa maana hapa Mahakama za Mkoa kwamba adhabu yake ya kifungo haizidi miaka 7 lakini mapendekezo ya sheria hizi kwamba adhabu itakuwa zaidi ya miaka saba na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mtapata fursa vile vile kuangalia hili kama miaka saba au zaidi ya miaka saba, kwa mfano inawezekana miaka saba mpaka kumi na nne inatosha haitoshi. Kwa hivyo mtakua na fursa na nyinyi kujadiliana na hili tuweze kufikia lengo halisi, lakini sambamba na hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine ambayo tumeyazingatia masuala ya kujamiiyana nayo haya katika mapendekezo yetu tumeona kwamba ni vyema yasiwe na dhamana tukifanya hivi tunaelea kwaba tnaweza kufikia hatua ya kuondosha udhalilishaji wa wanawake na watoto au kukomesha zaidi Zanzibar.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe, naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba sheria hii ina mapungufu na italetwa barazani ili tuifanyie marekebisho mimi nilitaka kujua kwa hivi sasa mwendelezo wake umefikia hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Kama nimemsikia vizuri Mhe. Panya ni kwamba anataka ajue hatua ambayo sheria hizi zimefikia.

Mhe. Mwenyekiti, hatua hizi kama nilivyojibu katika suala mama ni kwamba zimefikia katika hatua za mwisho mwisho, kwa hivyo tunatarajia muda wowote kama nilivyosema awali kipindi cha mwaka wa fedha ujao tutaleta hapa barazani, kwa hivyo hatua za mwisho kwa hivyo zitabakia zile ngazi kubwa kubwa tu ili iweze kufikia hatua ya kuletwa barazani Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea naomba tuwatambue wageni wetu wa leo hawa ni wageni wa Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na ni wanamichezo wa riadha wa Timu ya Taifa ya Zanzibar, wageni wenyewe ni hawa wafuatao.

Kwa upande wa viongozi

(1) Abdulahakim Cosmas Chasama Mwenyekiti wa ZAA
(2) Makame Mshimba Mbarouk
(3) Suleiman Ame Khamis Katibu Mkuu ZAA
(4) Muhidin Yassin Masusti Meneja
(5) Mwaka Mrisho Abdalla Mjumbe wa Kamati Tendaji hao ni upande wa viongozi.

Sasa kwa upande wa wachezaji.

(1) Omar Rashid Said
(2) Najim Ali Hamad
(3) Abdultalib Kheri Simai
(4) Abdalla Jecha Abdalla
(5) Dau Dahala Sheha
(6) Lulu Richard Kanua
(7) Kazija Hassan Simai
(8) Sharifa Shamsi Mara
(9) Zuleha Omar Kombo
(10) Asha Abdalla Khatib

Karibuni sana.

Nam. 76

Kuzuiliwa kwa Mzigo wa Kokoto Uliopita Bandarini Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Mnamo tarehe 16/03/2017 kulishushwa kokoto za kujengea kutoka meli ya mizigo iliyotoka Dar-es-Salaam. Gari zipatazo 15 zilitumika kupakia mzigo huo ambapo gari 12 ziliruhusiwa kuondoka bila usumbufu wowote lakini gari 3 zikazuiliwa na Afisa wa Kilimo.

(a) Je, ni sababu gani gari hizo 12 zikaruhusiwa na nyengine 3 zikazuiliwa.

(b) Kwakuwa kuna taarifa kuwa wamiliki wa mzigo huo wamelipishwa fedha kiasi cha shilingi 1.0 milioni ni sababu gani wamiliki hao wakalipishwa.

(c) Je, ni nani wamiliki wa mzigo ule wa kokoto.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Idara Maalum za SMZ (Kny: Waziri wa Kilimo, Mifungo, Maliasili na Uvuvi) - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuayavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2015 inamtaka kila anayechimba kukwangua, kuuza au kusafirisha mali asili zisizorejesheka ikiwemo kokoto awe na kibali cha kufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, siku ya tarehe 16 Machi, 2017 Maofisa wa Ukaguzi wa Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka waliopo bandarini, walikamata shehena ya kokoto tani 1,299 za bwana Nassor Saleh Ali, mkaazi wa Zanzibar ambazo zilikuwa zinatoka Tanzania Bara. Jumla ya magari 15 yanakisiwa yalitumika kusafirisha kukoto hizo kutoka bandarini na kuzipeleka Kiwanda cha Sukari Mahonda.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya magari hayo 15 yaliyokuwa yakisafirisha kokoto hizo, magari 3 yalizuiliwa katika Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka Marumbi yakiwa ni kielelezo cha kokoto hizo ambazo zilikuwa zikisafirishwa bila ya kibali halisi cha serikali. Kwani muhusika hakuwa na dhamira ya kulipa ada ya usafirishaji huo, baada ya kuzuiliwa magari hayo muhusika alitakiwa kulipa ada ya usafirishaji ya jumla ya shilingi 1,200,099 sawa na shilingi 1000 kwa tani moja. Muhusika alilipa kwa risti Nam. S/H259010 na kuruhusiwa kuendelea na kusafirisha kokoto hizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nifafanue kuwa kilicholipwa hapa ni ada ya usafirishaji wa kokoto tani 1,200,099 na sio idadi ya magari, mzigo huu ungeweza kubebwa na gari idadi yoyote muhusika anayopenda alimradi tani zilizobebwa zimelipiwa kibali. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri Mhe. Jaku Hashim kwa swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti Kaimu Waziri wa Kilimo kuwa tayari kupokea masuala mawili madogo ya nyongeza.

Ulipokuwa ukijibu suala la msingi hii sheria sijui ilikuwa imelala kwanza kwa ajili ya Ramadhani muda mrefu ni mtu mmoja tu kukamatwa na hizi kokoto na Afisa Mali asili walikuwa hawapo hii kadhia nimeikuta nikuwa ninakwenda zangu Dar-es-Salaam wakawa wanazozana watu na nimeshuhudia kokoto zikiletwa mara nyingi hakuna kuchajiwa. Sheria ilikuwepo wapi na hawa niwaekezaji wanajenga Kiwanda cha Sukari Mahonda hatuoni kutokuwapa moyo kokoto, kwa wawekezaji wale kufungua kiwanda kile ambacho kimefanya kazi kubwa sana na niwapongeze kwa kazi waliofanya kiwanda kile.

Ni sababu gani za msingi mtu huyu mmoja keshaleta kokoto karibu miaka 15 hajaulizwa chochote sheria lilikuwepo wapi, hivi sasa kwenda kukamatwa gari zake 3 za mwisho tena sifahamu sababu gani.

1. Tokea kuwepo Waziri Hamad Rashid mambo ya ajabu yanatokea na yataendelea kutokea Mungu akitujaalia, kaanza na mchanga kaja na kokoto. Kokoto zinatoka wapi Rufiji sijui wapi kesho kutwa atataka makaa yalipiwe na majivu yalipiwe ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub uliza swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haoni Mhe. Waziri ni kuwabana wazalendo Wazanzibari, nasema tena ni wazo la haraka hapo nyuma sheria ilikuwako wapi, karibu miaka 15 mtu huyo analeta kokoto na biashara yake hajaulizwa hata sikio wala ndevu. Sababu gani zilizopelekea sheria hiyo kulala baadae akaambiwa akalipe pesa hizo na hizi kokoto za wawekezaji.

2. Tokea kuwepo Mhe. Hamad Rashid kuna mambo ya ajabu yanatokea katika wizara hii hapo nyuma hayakutokea, ikiwemo mchanga, kokoto kesho atakuja na majivu kesho atakuja na kome zilizopakiwa mle ndani zilipiwe ni sababu gani ya msingi, hamuoni ni kuwabana Wazanzibari kuendelea na majukumu yake ya kikazi na ajira yenyewe ikawa haipo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (Kny: Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Kwanza sheria ni sheria kasoro ya utekelezaji wa Sheria haimfanyi anayekamatwa na kosa kutokuchukuliwa hatua za kisheria. Kwa mfano, miaka 15 aliyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub, mtu yeyote akikamatwa na hatia wakati ule ndo anahesabiwa kwamba anatuhumiwa na amekamatwa na kosa. Sasa lakini nataka nimfahamishe Mhe. Jaku kwamba mfanyabiashara yoyote kama nilivyosema kwenye jibu langu mama kwamba mambo ambayo yameelezwa ndani ya Sheria ya Maliasili zisizorejesheka, hasa usafirishaji wa kokoto tena zinazotoka Tanzania Bara inatakiwa hizo lazima zilipiwe ada ya usafirishaji. *(Makofi)*

Serikali ilichofanya ni kumtoza ada ya usafirishaji na kwanza nataka nimfahamishe, waliokamatwa na kokoto sio Kiwanda cha Sukari kwa maana ya Muekezaji ni *supplier* ambaye amepewa kazi na Kiwanda cha Sukari na *supplier* yoyote kwa mujibu wa sheria zetu za nchi, anatakiwa alipe ada na kodi zote za serikali huyu hakuwa amelipa ada na ndio maana akatozwa kulipia ada ya usafirishaji kwa hiyo serikali haioni kwamba hapa imewabana wafanyabiashara wazalendo isipokuwa imemtaka afuate utaratibu kwa mujibu wa sheria ya nchi. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Mhe. Ali Suleiman Ali, kwa swali la nyongeza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia hapa kwetu kadhia kubwa ya maeneo yetu ya miundo mbinu kwenye mazingira yetu kwenye kokoto, kifusi pamoja mchanga kwamba ni madogo na yanaathirika siku hadi siku. Na kwa kuwa swali hili limeuliza, nimejibiwa kwamba kuna mfanyabiashara au muwekezaji kaingiza kokoto kutoka Bara na hiyo ni moja wapo kunusuru maeneo yetu madogo kwa kuwa wenzetu wametukubalia kuingia hapa bila ya matatizo.

Je, wizara kwa kuzingatia usalama wa maeneo yetu haiyoni kwa hivi sasa imefika wakati kuwaruhusu wananchi au wawekezaji kutoa bidhaa hizo Bara bila ya ushuru, ili tunusuru maeneo yetu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (Kny. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Mwenyekiti naomba arejee lile swali la mwisho.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Suleiman Ali, naomba urejee.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. nimesema vipi la mwisho, la mwisho nimesema hivi ili kunusuru maeneo yetu kwenye mchanga, kokoto ama kifusi haioni serikali au wizara umefika wakati sasa kuwaruhusu bidhaa hiyo bila ya ushuru wowote kwa kuwa kule kainunua kuingia hapa kwetu kuwasaidia wananchi wetu na kulinda mazingira yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (Kny. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa Kijitoupele swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa sheria na leo hii Mhe. Waziri wa Fedha na kesho tutapitisha sheria nyengine zinazohusiana na masuala ya fedha na kodi. Mimi nadhani jambo alilioliuliza Mhe. Mwakilishi ni jambo ambalo linahitaji zaidi mazingatio ya Kisheria, kwa sasa hivi sheria zetu zinamtaka kila anayesafirisha au kuingiza bidhaa alipe kodi au alipe ada ambayo imewekwa kwa mujibu wa sheria, pale ikakapoonekana nahaja ya kufanya hivyo basi utaratibu wa Kisheria upo wa kuomba kwa Waziri wa Fedha kupata msamaha wa kodi au ada inayohusika kwa Waziri muhusika.

Lakini, kwa sasa tunawaomba wananchi na wafanyabiashara waendelee kufata sheria, ili serikali iendelee kupata mapata mapato yake. Ahsante sana.

Nam. 99

Uhaba wa Daktari Bingwa wa Mifupa Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la ajali za barabarani zinazosababisha vifo, vilema na majeraha mabaya. Pamoja na ongezeko hilo la ajali bado Hospitali ya Mnazimmoja kuna daktari bingwa mmoja tu wa mifupa katika kitengo cha dharura ambaye hatoshi na mara nyingi inapotekezea mahitaji hulazimika kutafutwa, kwa vile hawezi kuwepo kwa saa 24.

Je, kwanini juhudi za makusudi zisifanyike kutafuta daktari mwengine wa mifupa, ili kukabiliana na uhaba uliopo hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 99 kama ifuatavyo:-.

Kwa ruhusa yako Mheshimiwa kabla ya kujibu swali hili naomba nitowe maelezo kidogo kwa faida ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba kuna ongezeko la ajali za barabarani ambazo husababisha ulemavu kwa wananchi uharibifu wa mali za wananchi na kupata majeraha makubwa ambayo *final* hupelekea vifo na kuleta huzuni kubwa kwa jamii na taifa letu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwakubusha na kuwaomba wananchi wote watumiaji wa vyombo vya usafiri na watumiaji wa barabara, hususan vijana wetu kwamba maisha yenye afya yanathamani kubwa kwetu. Hivyo, tuwe makini sana huku kila mmoja wetu huwa na dhamira ya dhati ya kulinda maisha yake na maisha ya watumiaji wengine bila ya kujali kwamba mwenzake anatumia baiskeli au anatumia rikwama au anatembea kwa miguu au usafiri wa vyombo vya moto. Kwani sote tuna haki na wajibu wa kutumia barabara kwa usalama kwa faida yetu na taifa kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inatumia fedha nyingi ili kuokoa maisha ya wananchi wake kutokana na ajali za mara kwa mara ambazo ajali nyingi hutokea kutokana na uzembe wa utumiaji mbaya wa barabara na kuisababishia serikali hasara na kupoteza nguvu kazi ya taifa, kwani asilimia kubwa ya wanaopoteza maisha ni vijana ambao ni tegemeo kubwa kwa taifa la baadae.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba nijibu swali kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kitengo hichi kilikabiliwa na uhaba wa wafanyakazi wakiwemo wataalamu hii ilitokana na tatizo la uhaba wa wafanyakazi tulilokuwa nalo, katika baadhi ya vitengo vya Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, tunaishukuru sana juhudi za serikali yetu chini ya uongozi imara wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, kutoa kipaumbele kwa Wizara ya Afya kuweza kuajiri wafanyakazi wakiwemo wataalamu mabingwa wa fani mbalimbali kikiwemo Kitengo cha Mifupa.

Hivi sasa kitengo hichi kila jumla ya wafanyakazi kumi na moja (11), wakiwemo madaktari saba (7) na madaktari wengine wa kawaida ambao wamepatiwa mafunzo na wapo chini ya usimamizi wa madaktari bingwa na ambao hutoa huduma hospitalini kwa masaa 24. Wizara imewapeleka masomoni madaktari bingwa wa kitengo hicho wawili (2) na tuna mpango wa kuwapeleka wengine zaidi ili kuondosha kabisa upungufu wa wataalamu na kuendana na kasi mahitaji ya huduma katika kitengo hichi ambacho kinashughulikia, ambacho licha ya kushughulikia majeruhi wa ajali pia kinashughulikia wagonjwa wa sukari ambao kwa bahati mbaya hupelelekea kupoteza viungo vyao, kinashughulikia watoto wanaozaliwa na ulemavu ambao huhitaji kufanyiwa matengenezo ya viungo vyao, kwa mfano wale watoto wenye miguu rungu na kadhalika. Ahsante Mhe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nipokee majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwa masikitiko na nimpongeze Waziri kwa ziara ya aliyoifanya ya kushtukizia hivi majuzi hasa katika sehemu ya wazazi na kaiona mwenyewe kuliko kuja kuuziwa mbuzi kwenye gunia, kaiona hali halisi mwenyewe akasikitika sana kwenye vyombo vya habari.

Mhe. Waziri nilikupongeze kwa dhati na haya ndo uwajibikaji unaofanya na nikuombe Naibu Waziri kasema saa 24 huduma zinazopatikana hapo kwa Mungu hazipo masaa 24. Kwa hiyo nenda pale kaangalie mpaka daktari apigie simu kama hamna gari uchukue gari tia tukuta kwa hiyo mkayajibu majibu Mhe. Waziri na wengine Waziri na Manaibu Waziri jaribu kufuatilieni mnachoulizwa.

(a) Lakini mgonjwa anapofika pale huduma ya *X-ray* ikiwa ya mifupa, kavunjika mfupa kakatika mfupa huwezi kutibia bila ya kupiga *X-ray*, sababu gani za msingi iliyopelekea pale ukaandikiwa tangazo hasa *X-ray* haipo. Ni sababu gani za msingi suala dogo sana hilo, mwananchi katoka vijijini kufika pale anaambiwa huduma ya *X-ray* haipo hana pesa mtibabu bure au matibabu pesa.

(b) Vilevile, huyo mgonjwa Kitengo cha *X-ray* kiko juu, ni sababu gani mgonjwa huyu kuchukuliwa kama mzigo wa kuni au pakacha la makaa kupelekwa juu wakati *lift* haifanyi kazi, ni muda gani *lift* hiyo haifanyi kazi nini matarajio kwa Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, tatizo la kuwambiwa *X-ray* haifanyi kazi Mheshimiwa hili ni tatizo la kawaida, *machine* ni kama binaadamu inaweza ikafanya kazi sasa hivi lakini muda huu ikaharibika.,

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Kaa kuhusu utaratibu nimekuona kwa sababu Mhe. Naibu Waziri bado anaendelea kukujibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kwa hio Mhe. Mwenyekiti inawezekana wakati alokwenda yeye mgonjwa kufanyiwa kipimo hichi cha *X-ray* ikawa machine wakati huo imegoma kutokana na matatizo ya kawaida kama *machine* kama binaadamu ambaye inafanya kazi, lakini si wakati wote ambayo machine hii *X-ray* inakuwa haifanyi kazi na mtu anapokwenda mgonjwa si wakati wote anaambiwa *machine* haifanyi kazi. Iko wakati inafanya kazi na wakati wengine hii inazidiwa na kuweza kupumzika yeye mwenyewe *machine* kama *machine*. *(Makofi)*

(b) Kuhusu *lift* Mhe. Mwenyekiti, ile *lift* sote tunafahamu kwamba iliwekwa tangu lilipojengwa jengo lile la Mnazi Mmoja, kwa hiyo ni *lift* ambayo kwa kweli imeshachoka, tunachokifanya uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kuifanyia ukarabati kila mara inapogoma na inapofanya matatizo yake inafanyiwa ukarabati.

Hata hivyo Wizara tuna mpango mkubwa baada ya kutengeneza lile jengo na *lift* pia kuwekwa mpya sio moja, tutaweka *lift* zaidi ya moja. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Seif Abeid kwa swali la nyongeza.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwakuwa, kwenye majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kuna mpango wa kuwapeleka na wanawasomesha madaktari bingwa 2 wa mifupa, ambao watasaidia wataongeza nguvu kupunguza hilo tatizo hilo la lililozungumzwa kwenye swali la msingi na kuwa na sisi Pemba tatizo hili lipo, mimi nilitaja nijuwe jee baada ya kurudi hao madaktari bingwa wa mifupa 2, Wizara ina mpango gani wa kumpeleka mmoja Pemba katika hospitali ya Abdalla Mzee ambapo hapo zamani ilikuwa maarufu mtu akianguka mkarafuu akipata ajali kubwa unaambiwa unakimbizwa Mkoani huyo Abdalla Mzee.

Na sasa hivi kidogo inaonekana kama ile hadhi ya watu kama wale kupata matibabu kama yale yamepungua, niliomba nijue serikali ina mpango gani baada ya hawa kurudi kwamba mmoja wao atapelekwa Mkoani kwenda kuengeza nguvu pale ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, niliseme kwenye jibu langu la msingi kwamba tunawafanyakazi wataalamu wawili wapo kwenye masomo, lakini kuna wengine ambao wakirudi hao tutapeleka wafanyakazi wengine. Nakuahidi kwamba kupitia wafanyakazi hawa wawili ambao wapo masomoni huenda tukawepeleka wote katika hospitali ya Abdalla Mzee au huenda tukampeleka mmoja kulingana na mahitaji. Kwa sababu kwa sasa hospitali ya Abdalla Mzee kuna wafanyakazi wawili mmoja ni mzalendo na mmoja ni mgeni. Kwa hivyo huenda tukaongeza nguvu pale ya mfanyakazi mwengine mtaalamu mmoja ili walingane na hospitali ya Chake Chake na Hospitali ya Mkoani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nimekuona kuhusu utaratibu naomba ukae tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwahiyo, hutonipa tena au vipi.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh! Naomba ukae. Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa swali la nyongeza la mwisho.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana ya serikali, naomba kuuliza swali moja lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwasababu Mhe. Waziri amekiri kuwa kumetokea ajali nyingi na kunapokelewa majeruhi wengi kwa kila siku.

a) Je, serikali ina mkakati gani wa kufanya wodi maalum kama ya Moi iliyokuwepo Muhimbili.

b) Kwasababu amekiri kuwa *X-ray* mara inafanya kazi mara haifanyi kazi, tuna *X-ray* ngapi pale lakini na *lift* si tuliambiwa kwamba ilinunuliwa mpya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, suala la wodi maalum ya wagonjwa wa ajali limo sana kwenye mipango yetu na mara tutakapokamilisha ujenzi wa hospitali yetu basi wodi maalum ya wagonjwa hao itakuwepo lakini kwa sasa wangojwa hao pia tumewaweka katika sehemu maalum ambayo hawachanganyiki na wagonjwa wa maradhi mengine.

b) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa lift kama nilivyosema. Mheshimiwa samahani naomba arudie swali (b)

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Swali (b) nimesema kwa sababu mashine za *X-ray* zimekuwa mbovu mara nyingi tuna mashine ngapi za *X-ray* na vile vile lift hii tuliambiwa imenunuliwa mpya *lift* ile mpya imekwenda wapi hata tunasema ya zamani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti kwa sasa tuna mashine moja ya *X-ray* ambayo inafanya kazi, zipo nyingi lakini nyengine hazina uhakika hazifanyi kazi vizuri lakini inayofanya kazi inayo (*operate)* kila siku kwa uhakika.

Kuhusu *lift* sikumbuki katika jibu langu kama nimesema kwamba tumeshanunua *lift*, nimesema mara tutakapomaliza tumekusudia kuweka *lift* katika jengo letu lile.

Nam. 114

Uwepo na Matumizi ya Maeneo ya Wazi Katika Mji wa Chakechake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein inastahili pongezi kwa juhudi za kuiletea maendeleo Zanzibar na hasa katika Mji wa Chakechake ambao ni Mji wa pili wa Zanzibar kwa kuupandisha hadhi. Hatahivyo, miongoni mwa sifa za miji ni kuwa na mambo mengi kutokana na hadhi yake.

(a) Je, serikali imetenga maeneo mangapi ya wazi kwa ajili ya matumizi tofauti tofauti katika Mji wa Chakechake.

(b) Je, serikali inaweza kulifanya/kuligeuza eneo la Tibirinzi mkabala na jengo la Hoteli ya *ZSSF* kutumika kama forodhani ya Chakechake.

(c) Kama serikali imetenga au haijatenga maeneo ya wazi katika Mji wa Chakechake, haioni umuhimu wa kuyazuwia maeneo yote yaliyo wazi kujengwa majumba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 114 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo**:-**

Mji wa Chakechake ni mji wa pili kwa ukubwa Zanzibar. Kama ilivyofanywa kwa Mji wa Zanzibar, Mji wa Chakechake nao unatayarishiwa "*Master Plan"* yake. Ndani ya Mpango huo, maeneo yote ya wazi makubwa na madogo yataainishwa upya, ili yapate kujulikana yote na wapi yalipo. Kwa sasa maeneo yanayojulikana vizuri ni yale maaneo makubwa tu mfano, eneo la Gombani ya Kale, eneo la Chunjuu karibu na "*Fire*" na eneo la Tibirinzi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpongeze sana Waziri kwa majibu yake mazuri kwa sababu anataka kufanya *plan* ya Mji wa Chakechake lakini na mimi nitoe tu maelekezo kwenye suala la (a) na (b).

a) Kwakuwa nasubiri *plan* lakini wakati mwengine unaweza ukasubiri *plan* ukaona watu wanajenga je, Mhe. Waziri ananihakikishia kwamba hakuna ujenzi utakaojengwa katika maeneo hayo mpaka *plan* itakapotoka.

b) Ni kwamba katika eneo la Tibirinzi ni maeneo karibu na Ikulu na iko sehemu moja ambayo ilikuwepo Ikulu ya zamani ambayo inaitwa Ikulu ndogo. Je, haoni kama pakijengwa maghorofa itakuwa ni ile kazi ya kuja kuchungulia Ikulu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo ni kwamba hakutakuwa na ujenzi wa aina hiyo kwa sababu Wizara ya Ardhi ikishirikiana na Manispaa ya Mji tutakuwa tunaratibu na kuona kwamba hakuna shughuli ya ujenzi inayoendelea katika maeneo haya ya wazi.

a) Lakini pia nikuombe kama wewe utabaini ujenzi unaendelea katika eneo lolote la wazi tupe taarifa ili hatua zichukuliwe. Kwa jibu hilo imani yangu nafikiri kuwa umeridhika nalo.

b) Hakutakuwa na jengo lolote ambalo litakalojengwa na kuweza kuchungulia Ikulu. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pia napenda nichukue fursa hii niipongeze sana serikali kwa nia yake njema ya kutaka kuanzisha Mji wa Chakechake ambao utakuwa ni mji wa pili kwa Zanzibar.

Mara nyingi tunapoanzisha Miji tunatakiwa iendane na *business center*, ili wananchi wetu wapate huduma bora katika eneo moja la mji.

a) Je, katika mpango wa serikali jambo hili tumelizingatia.
b) Kama tumelizingatia suala la *business center* ni lini serikali itaweka wazi mpango wa ujenzi wa *business center* hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, ni sahihi kama alivyosema na hiyo *business center* ikionekana katika hiyo *master plan* na kwa upande wa Unguja tayari ipo lakini sasa tunaizungumzi ni utayarishwaji wa Kisiwa cha Pemba. Baada ya kukamilika kwake pia nayo itaonekana kama ilivyokuwa tayari kwa Unguja. Ahsante sana.

Nam. 45

Utaratibu wa Kuwapata Wakandarasi Wazalendo

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:

Pamoja na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwaondoshea changamoto wananchi wetu kwa kuwawekea mazingira mazuri ya miundombinu ya barabara ikiwemo ukarabati wa barabara hizo.

(a) Je, ni taratibu gani zinazochukuliwa ili kuwapata wakandarasi wazalendo wenye sifa za kupewa kazi hizo za ukarabati wa barabara zetu kwa kutumia kampuni za ndani.

(b) Je, wizara haijawa na utaratibu wa kutoa kipaumbele kwa kampuni za wazalendo zenye sifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 lenye vipengele (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kampuni nyingi za ndani hapa Zanzibar zimejikita zaidi kwenye miradi ya ujenzi na matengenezo ya nyumba ambayo inatofautiana na ile ya barabara. Aidha, siku hizi baadhi ya wananchi wameanza kuingiza nchini baadhi ya zana za ujenzi wa barabara lakini kwa

matumizi yao binafsi. Hatahivyo, kuwa na zana pekee haimaanishi kuwa kampuni tayari inazo sifa za kuitwa kampuni ya ujenzi. Ili Kampuni iwe na sifa za kuitwa kampuni ya ujenzi ni lazima isajiliwe kwa mujibu wa sheria za nchi, iwe na wataalamu wa kutosha na wenye weledi waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Watalaam, iwe na vitenda kazi au zana za kutosha na iwe na uzoefu wa kutosha unaolingana na kazi husika (mfano: ujenzi wa barabara, majengo, umeme, maji nk) lakini pia iwe inajimudu kifedha.

Mhe. Mwenyekiti, zipo baadhi ya kazi za matengenezo ya barabara ambazo hazihitaji mtu kuwa na taaluma ya kutosha bali kusimamiwa na kupewa maelekezo tu. Hatahivyo, msimamia ni lazima awe na taaluma ya uelewa wa kazi zinazofanyika. Kwa mfano wa kazi hizo za kawaida *(Routine maintenance)* ni kama vile ukataji wa majani/vichaka, miti, kusafisha mitaro, mchanga barabarani, madaraja na *culverts*. Aidha, zipo kazi za matengenezo ya barabara ambazo ndizo nyingi zinazohitaji Kampuni kuwa na zana/vitendea kazi vya kutosha, wataalamu wenye weledi na uzoefu wa kampuni wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, mfano wa kazi hizo ni matengenezo ya muda maalum *(periodic maintenance)* kama vile kuongeza tabaka la lami *(overlay/reseal)* kwenye barabara kongwe ili kuiongezea barabara muda wa kutumika, kuweka kifusi *(light or heavy grading*) na kukishindilia vizuri kulingana na maelekezo ya michoro au mtaalamu husika. Matengenezo kwenye sehemu korofi *(spot improvement)* mfano kujenga upya (*reconstruction*) kipande cha barabara kisichozidi kilomita moja ambacho mara kwa mara kinapofanyiwa matengenezo huharibika kutokana na ama kasoro wakati wa ujenzi, eneo lenye unyevunyevu *(swamp area)*, upitishaji wa mizigo mizito kuliko uwezo wa barabara *(overloading)*, barabara kutofanyiwa matengenezo kwa muda mrefu *(lack of maintenance)*, mabadiliko ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya asilimia thamanini (80%) ya kazi zote za matengenezo ya kawaida ya barabara *(routine maintenance)* ya mtandao wa barabara za lami *(road network for paved roads)* ulio chini ya majukumu ya wizara yangu, hufanyiwa usafi na vikundi vya kijamii na kampuni za ndani kwa kushindana. Kazi za matengenezo ya muda maalum, matengenezo kwenye sehemu korofi, kazi za dharura nk, zinahitaji wataalamu wenye weledi wa kutosha, zana maalum na uzoefu wa Kampuni wa kutosha. Karibu asilimia sitini (60%) ya kazi hizi hufanywa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB) na nyingine hutangazwa na kupewa Kampuni zenye sifa kwa mujibu wa taratibu za sheria ya nam 9 ya mwaka 2005 ya Manunuzi na Ufilisi wa mali za Umma pamoja na kanuni zake. Hata hivyo, kila miaka ikisogea, Idara ya UUB inazidi kupungua uwezo kutokana changamoto ya uchache wa zana na mitambo kutokana na mitambo na zana nyingi kuchakaa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia Bodi ya Usajili wa Kampuni Zanzibar *(Zanzibar Contractors Registration Board)* iliyo chini ya wizara yangu, imeweka utaratibu wa kutoa mafunzo mbalimbali kwa kampuni za ndani yanayohusu mambo ya miradi ya ujenzi. Mafunzo hayo ambayo huandaliwa na bodi hiyo mara moja kwa mwaka, huleta wakufunzi wa waliobobea kwenye masuala ya miradi ya ujenzi pamoja na kuwashirikisha wataalam kutoka *PBZ, TRA* na *ZRB* kwa lengo la kuzipa kampuni zetu uelewa na uwezo wa kuwa na kampuni yenye sifa, ili

waweze kupata kazi zinazotolewa na serikali, ambazo zote hutolewa kwa kufuata taratibu kama nilivyosema mwanzo za Sheria nam. 9 ya mwaka 2005 ya Manunuzi na Ufilisi wa Mali za Umma na wataalam wenye weledi kwenye masuala ya ujenzi. Zipo kampuni chache za ndani zinazofanya kazi ya matengenezo ya barabara hasa ya ujenzi wa madaraja, *culverts* na ukataji wa majani na kampuni moja tu ndiyo inayofanya kazi za matengenezo ya muda maalum ya barabara kwa kiwango cha kifusi tu ambayo ina zana za kutosha lakini haina wataalamu wa kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haina utaratibu mwingine wa kutoa kipaumbele kwa kampuni wa ndani kwa kuwapa kazi kinyume na utaratibu wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Nam. 9 ya mwaka 2005. Utaratibu huu utaendelea hadi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakapopitisha utaratibu mwingine. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jibu refu la Mhe. Waziri kwa mujibu wa Kanuni ya 37 lijibiwe jibu fupi na lenye ufasaha.

a. Ni kampuni gani iliyopewa nafasi hiyo ya kutengeneza barabara ya kifusi.
b. Je, kampuni hiyo iliyopewa kutengeneza barabara ya kifusi ina vifaa vya kutosha lakini haina wataalamu tumewezaje kuipa kazi kama hiyo ambapo inakosa sifa ya kuwa na wataalamu katika ujenzi wa barabara ya kifusi huoni hapa ni kupoteza fedha za serikali kwa ujenzi wa chini wa kiwango.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, napenda kushukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Kampuni yenyewe ni *Salim Civil Contractor* ndiyo waliyopewa hiyo kazi na walifanya barabara ya Kinduni kwenda kitope na kama nilivyosema mwanzo walikuwa kwenye usimamizi wetu wa wataalamu wetu wa UUB kwa hivyo baadhi ya kazi tunawapa wao kwa sababu tunakuwa na kazi nyingi lakini wasimamizi wetu wanakuwa pale kuhakikisha kwamba ile kazi inafanyika kwa mujibu wa viwango tunavyovitaka.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwa kuniona nami kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na mimi naomba nimuulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara yake katika majukumu yake moja ni kuwaendeleza wakandarasi wazalendo. Je, niwakandari wangapi mpaka sasa ambao wamewaendeleza.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mheshimiwa utaratibu, nimeuliza maswali mawili (a) na (b) nimejibiwa swali la (b) swali la (a) mbona sijajibiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani nimekuona kuhusu utaratibu lakini naona amesema anakujibu yote kwa pamoja, yaani ameunganisha jawabu lake kwa swali lako (a) na (b) kwa pamoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Sisi kama tulivyosema mwanzo kazi yetu ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na wataalamu wa kutosha ambao wana viwango. Mara ya mwisho miezi miwili iliyopita mimi nilikwenda kuyafunga mafunzo yao lakini kama nilivyosema mwanzo ili upate kuwa na sifa hizi ni lazima kwanza upasi mitihani ambayo unatakiwa upasi na baadaye upitishe na bodi yetu ya usajili. Kwa hivyo hiyo ndiyo taratibu zetu zinavyokuwa na baadaye ndiyo tunapata kujua wataalamu wangapi walio-*qualify* lakini ni kazi ngumu kwa sababu siyo watu wengi wanaokwenda kusomea masomo ya *engineering* wengi wanapenda kusoma masomo ya *art*.

Napenda nitumie nafasi hii kuwaomba sana Wawakilishi washajihishe wapiga kura wao wapate kusomea masomo ya sayansi kwa sababu kuna fursa nyingi za ajira katika mambo ya utaalamu huu wa *engineering*. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 56

Ajira za Wazanzibari Katika Shirika la Ndege la *Air Tanzania Cooperation*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani (Kny: Simai Mohamed Said) - Aliuliza:

(a) Wazanzibari wangapi wameajiriwa katika Shirika la Ndege la *Air Tanzania Cooperation*.

(b) Ni nani aliyenunua ndege hizo mpya za *Air Tanzania Cooperation* na kiasi gani cha mgao wa fedha Zanzibar itapata.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Shirika la Ndege la Tanzania (*ATC*) limeajiri Wazanzibari watatu (3) mpaka hivi sasa.
(b) Ndege za Shirika la Ndege la Tanzania limenunuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Mwenyekiti, hakuna fedha inayokuja Zanzibar moja kwa moja hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inanufaika na mambo yafuatayo kutokana na ununuzi wa Ndege hizo:

1. Ajira kwa Wazanzibari
2. Kuleta watalii visiwani mara tano kwa wiki (kupitia Kilimanjaro)
3. Kusafirisha abiria wa kawaida kwenda Zanzibar na kuondoka Zanzibar. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri lakini tuliambiwa katika taasisi zote za Muungano kuna 40% ya ajira. Je, kuwa na wafanyakazi watatu tu katika Shirika la Ndege la ATC huoni kwamba tunakiuka utaratibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kujibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli hivi sasa hili shirika ndiyo linataka kujiimarisha kwa hivyo katika njia za kubana matumizi na vile vile kutaka kupata faida kwa ajili ya kubana matumizi na vile vile kutaka kupata faida kwa ajili ya kuliendeleza hili Shirika kuitangaza Tanzania zaidi limeamua kuwapunguza baadhi ya wafanyakazi na kubakia na wafanyakazi weledi ambao wako tayari kujituma na kufanya kazi masaa 24 ili kuhakikisha kwamba hili Shirika linajiendesha kibiashara. Kwahivyo, wafanyakazi watatu wawili wapo Unguja na mmoja Pemba kwa hivi sasa ni wafanyakazi wanaotosha mpaka hapo Shirika litakapozidi kujiimarisha kiuchumi zaidi na kupata faida basi uwezekano wa kuongeza wafanyakazi utakuwepo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Makasio na Matumizi ya mwaka 2017

(Kusomwa ya mara Pili)

Mhe. Mwenyekiti: Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena naomba nitimize wajibu wa kikatiba chini ya kifungu cha 106 kinachomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha katika Baraza la Wawakilishi Mswada kwa ajili ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kila mwaka unapoanza.

Kwa heshima, kubwa naomba sasa kwa ruhusa yako niwasilishe mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya Shilingi Trilioni Moja Bilioni Thamanini na Saba Milioni Mia Tatu Hamsini na Tisa na Laki Nne (1,087,359,400,000) kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaishia tarehe Thalathini Juni, Mwaka Elfu Mbili na Kumi na Nane.

Pamoja na kuruhusu utowaji na uhaulishaji wa fedha hizo na mambo yanayohusiana na hayo...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri samahani kidogo kabla ya kuendelea naomba nimpitishe Mhe. Mwenyekiti aendelee na hii shughuli.

Mwenyekiti, (Mhe. Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Spika, Naibu Spika, nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti na nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa mashirikiano yako makubwa ambayo yametuwezesha sisi Wizara ya Fedha na Mipango kuandaa na kuwasilisha bajeti ya serikali ambayo kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018, kwa mara ya kwanza ilipitishwa na Baraza lako Tufuku mwisho baada ya kuchangia bajeti ya wizara zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyomalizia na bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Pili nawashukuru sana kwa mapenzi yenu kwa serikali na wananchi wa Zanzibar nasema bila ya nyinyi kukubali bajeti hii watendaji ndani ya serikali tusingeweza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuidhinishwa kwa bajeti ya wizara zote hizo kunapelekea Mswada wa Makisio na Matumizi kutowa uwezo kwa Serikali kutumia kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya shilingi mia tano tisini bilioni na mia saba na hamsini na nane milioni na laki moja (590,758,100,000) kutumika kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi mia nane tisini na sita bilioni mia sita na tano milioni na laki tatu (896,605,300,000) kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kupitishwa kwa mswada huu kutaiwezesha pale inapobidi Serikali kukopa ndani na nje fedha kwa ajili ya matumizi ya ndani kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018. Kiasi cha fedha kilichoainishwa kwa ajili hiyo ni kama kinavyoongozwa na masharti ya kifungu cha 5(1) cha mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu una vifungu 9 kifungu cha kwanza kinazungumzia jina fupi, kifungu cha pili kinazunguzia tafsiri, kifungu cha tatu utowaji wa shilingi trilioni moja bilioni thamanini na saba milioni mia tatu hamsini na tisa na laki nne (1,087,359,400,000) kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha nne kinazungumzia makisio ya fedha zilizobakia na kifungu cha tano chenye vifungu vidogo vinne kinazungumzia uwezo wa kukopa waziri mwenye dhamana ya fedha, kifungu cha sita chenye vifungu vidogo vitatu kinazungumzia uwezo wa waziri katika maombi ya ziada kwa lengo la kukabili matumizi mengine ya dharura pale haja inapotokezea.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha saba kinazungumzia marejesho ya mkopo na riba na kifungu cha nane kinazungumzia kukubaliwa kwa mipango ya maendeleo na kifungu cha tisa ambacho ni kifungu cha mwisho kinazungumzia kukubaliwa kwa fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo haya mafupi ya mswada huu naomba sasa kwa idhini yako kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe kujadili na hatimaye kuupitisha mswada huu ili iwe ni Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa mswada uko mbele yetu, kwahivyo tunaweza kuujadili.

Mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Miraji Khamis Mussa kwakuwa yeye ni Mwenyekiti hawezi kuleta hotuba yake nyengine, huu ataleta Mwenyekiti baadaye kwa mswada huu tunaendelea kuujadili moja kwa moja kwa mujibu wa kanuni zetu. Mhe. Miraji Khamis Mussa tafadhali.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia nikiwa mtu wa mwanzo lakini kwanza nimshukuru waziri kwa uwasilishaji wake.

Mimi Mhe. Mwenyekiti kwenye mswada huu katika eneo la kifungu cha 5(1) Uwezo wa Waziri wa kukopa. Ninakubaliana kidogo na maelezo yaliopo hapa lakini kwa mantiki fulani hayakuwa sawa, nilikuwa naomba tuu tuyaongeze ili kuweka sawa kwasababu uwazi ulipo katika eno hili inaonekana wazi kuwa tumeruhusu kukopa lakini kile tunachokikopa kwa mujibu wa bajeti tuliyoipitisha sasa hayakufungika hapa hii iko-*loose* maana anaweza akakopa kwa zile pesa ambazo tumeziidhinisha katika Miradi yetu ya Maendeleo maana kuna zile za serikali lakini kuna zile ambazo serikali itakopa kama mfano kupitia *Exim Bank* kupitia maeneo mengi ambayo tumeyaainisha. Kwahivyo, nilikuwa naomba tuu kuwe na marekebisho ya ziada kwa waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha anaweza kukopa wakati wowote ule sio zaidi ya tarehe 30 Juni, 2018.

Kuna maneno yaongezeke kwa zile fedha zilizopitishwa kwenye makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwenye Baraza la Wawakilishi kwa mwaka huu wa fedha hayo maelezo mengine yabaki kama vilivyo. Lakini katika kifungu cha 6(1) pia kuna maelezo waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha ataona ni manufaa kwa taifa kutowa matumizi ya ziada kwa wizara au idara za serikali ikiwa ni zaidi ya fedha zilizokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa kwa madhumuni ya huduma nyenginezo zozote na itakuwa si hasara kwa taifa, kunako eneo hili kipengele hiki mimi sikubaliani nacho sababu katika utaratibu wetu hapa Mhe. Waziri anaanza kutaka kunyima ile fursa lakini na muongozo wa kikatiba ulokuweko katika kama sikosei ibara ya 88 ya Baraza letu hili tukufu.

Kwasababu katika ibara 88 moja ya kazi zetu kwenye Baraza ni kujadili shughuli za kila siku za kila Wizara wakati wa kikao cha mwaka wa bajeti katika Baraza la Wawakilishi kifungu 88(b) lakini pia 88(d) kuidhinisha na Kusimamia Mpango wa Maendeleo wa Serikali katika njia ile ambayo bajeti ya mwaka inaidhinishwa, maeneo mawili haya sisi tutakuwa tunaidhinisha mpango wa Serikali ambapo mpango ndo unotufanya tupitishe bajeti yao sasa leo tunakimbia kile kipengele cha kuja na *supplementary budget* ambayo kazi ya Baraza la Wawakilishi kuja kujadili na kuidhinisha ile shughuli inayotoka serikalini.

Kwakuwa, mwaka wa fedha huu tumepitisha fedha kwa ile mipango ya serikali na Baraza hili sio tuu tukiondoka hapa halipo tena tunakuwa na Baraza kwa vipindi tofauti na matumizi ya serikali tuliyopitisha ndio tumeyapitisha kwa utaratibu wa mpango wa serikali sasa dharura hii ya

kifungu hichi tukiendelea kuweka wazi kwa waziri ana uwezo kwa kuidhinisha fedha maana yake tunanyima ile fursa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuja kuidhinisha, lakini nakumruhusu waziri aje apitishe kitu kinyume na ule mpango wa serikali tuloupitisha sasa mwisho huku akaielezea katika kifungu namba 2 ambacho baada ya hayo matumizi ikitokezea dharura hii atakuja kuwasilisha yale matumizi alikwisha yafanya baada ya huu uwezo tunaomkasimu hapa.

Leo tunampa uwezo huu lakini tunachosubiri sisi baada ya uwezo huu kumpa Waziri ambaye ni mmoja tuu katika wawakilishi wote tuliomo ndani ya baraza hili, tukisha mpa uwezo anakuja kutuambia sisi hii ripoti yenu ya matumizi tukiwa hatukuiyafiki na ule mpango hatukuwafiki atatuambia nini sasa haya yote mawili miye sikubaliana nayo na sikubaliani nayo kwa sababu nimesema katiba ya nchi inaturuhusu sisi kuja kujadili hili. Lakini katiba ya nchi inaturuhusu sisi kupitisha Mpango wa Serikali hiyo katiba leo tunataka kuidhinisha hili ambapo linakiuka yale mamlaka ya kikatiba kuwepo kwa chombo hichi, kwa hivyo kwenye eneo hili sikubaliana nalo lakini kwenye kifungu pia cha 6(3) kinasema tu Waziri mwenye dhamana na mambo ya fedha anaweza kukasimu uwezo wake alionao chini ya kifungu hiki kwa Afisa yeyote kwa mujibu wa masharti atakayoona yanafaa.

Narudia tena kwenye Katiba kifungu cha 43(4) (a) ambapo ni sehemu ukikipitia unakuta wazi pale kuwa pana majukumu ya Mawaziri, maana pale panazungumzwa Baraza la Mawaziri na ndio jukumu la Mawaziri mojawapo ni kumsaidia na kumshauri Rais. Jukumu hili Waziri analilia kiapo lakini leo tunataka kumpa mamlaka ya yeye kumkasinisha Afisa yeyote kitu ambacho huyo Afisa anamkasinisha kile kiapo cha kumsaidia Rais kwa mujibu wa katiba hii hakukila huyu, amekila waziri kwa madhumuni maalum ya kumsaidia Mhe. Rais leo tunatoka tunaicha katiba tunataka kwenda kuidhinisha jambo ambalo linakiuka katiba ya nchi kitu ambacho miye kwangu pia kunako eneo hili siafiki, siafiki kabisa sasa niombe maeneo haya hapa.

Lakini nende pia katika eneo la majadweli kunako Wizara ya Fedha na Mipango jadweli zilizokuwemo humu zinaonyesha *summary* ya fedha jadweli moja tuu jadweli lote limeenda vizuri jadweli hilo linazungumzia Usimamizi wa Bajeti ya Fedha za Umma. Kwenye kitabu hiki mwisho kuna sitini na nne bilioni mia nane na thalathini na nane *point* moja (64,838.1) hizi fedha ukienda katika kitabu kikubwa tulichokipigia kura ndiyo tunaitikia kule kuna tofauti ya kifungu hiki na fedha ziliopo kuna sitini na nne bilioni, laki nane na nane (64,000,800,008) huku leo tunapokea *summary* yenye sitini na nne mia nane thalathini na nane *point* moja (64,838.1) zote bilioni lakini hapa pana tofauti ya milioni thalathini (30,000,000). Milioni thalathini (30,000,000) hii kwenye kitabu maana kule tumepitisha ndogo hapa tumeidhinisha kubwa lakini hii hesabu huku chini inakuja *total* kwa utaratibu gani.

Kuna kifungu pia ambacho cha Uendeshaji na Utaratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango ambachio hiki ndani ya *summary* hii ina thalathini na nne bilioni milioni mia tano na kumi na nne (34,514,000) lakini kweye kitabu kikubwa tulichoidhinisha kina thalathini na nne mia tano na arubaini na nne (34,544,000) kwa hivyo hapa pana ongezeko na milioni thalathini (30,000,000) huku kuna punguzo huko ongezeko, lakini kihesabu maana yake zita-*total* kwasababu huku kapunguza huku kaongeza lakini tulichokipitisha kwenye Baraza hili

kinatakiwa kifuatwe kama kwenye kitabu kikubwa kilivyo, kwa hiyo *summary* yake hii hapa lazima akubaliane nami kufanya marebisho kutokana kwenye kitabu kikubwa tulichokipitisha kwenye wizara yake.

Baada ya maelezo hayo lakini naomba niseme Mhe. Mwenyekiti mimi kwenye maeneo hayo sitakubaliana nayo kupitisha kama tunataka kukiuka sehemu ya matakwa ya katiba ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri zaidi ya maeneo hayo naomba kuunga mkono kwa asilimia hiyo hamsini sina tatizo na Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mraji Khamis Mussa kwa mchango wako. Sasa namwita Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu na lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri na Watendaji wake kwa muda wote wa Baraza hili tumekaa kwa vizuri na salama kwa usalimini.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti niseme tuu kwamba mimi naunga mkono hotuba hii ni hotuba ambayo nzuri na tunadhhiirika kwamba wajibu wetu tuipitishe vyema ili Mhe. Waziri apate afanye kazi zake ipasavyo.

Hotuba hii Mhe. Waziri imekusanya mambo mengi lakini kubwa kuna vipengele vya katiba lakini miye niseme tuu kwa upande wangu mimi sina tatizo nalo nimuombe tuu Mhe. Waziri kwa kuwa hii ni dhamana nzito na roho ya nchi yetu inaitegemea nimuombe kwa dhati kabisa yeye na watendaji wake wote tuongeze bidhii na tuwe waadilifu katika kuhakikisha kwamba fedha zetu zinapatikana na tunadhiinisha lakini zitakota kwa kufanyia kazi zinatukabili katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la fedha hizi ni bajeti yetu kubwa kwa mwaka huu katika historia ya maisha yetu au katika historia ya Baraza lilivyoaanza tuna *trillion* yaani kufika kwenye *trillion* si jambo dogo. Kwahivyo, nimuombe Mhe. Waziri hili suala naamini kwamba panapopatikana mahitaji haya au fedha hizi kero zetu mbalimbali katika nchi yetu zitaondoka kwahiyo nimuombe tu Mhe. Waziri nimesimama hapa kwa muda mfupi kumuunga mkono na kuiunga mkono hotuba hii lakini pia na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, bado muda upo Mhe. Hamza Hassan Juma, tafadhali kuchangia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri kuhusu kuidhinisha ili tumpe nafasi akatumie pesa kwa ajili ya kutekelezwa yale yote ambayo tuliyoyajadili hapa katika kipindi chote cha bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naungana na mwenzangu mjumbe mwenzangu Mhe. Miraji Khamis Mussa zaidi katika kuangalia masuala ambayo yanayogusa moja kwa moja katiba na zile dhamana ambazo tunazokasimiana katika sheria zetu mbali mbali. Lakini kikubwa zaidi ni kuangalia *figures* ambazo zilizokuwemo kwenye kitabu kikubwa na zile *figures* ambazo tunazoziidhiinisha. Naamini Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wanatusikia watayaangalia hayo kama kunahitajika marekebisho inawezekana pengine *typing error*, inawezekana pengine kulikuwa kuna makosoe ya hapa na pale ili kile ambacho tunachokiidhinisha kiwe ni sahihi ili tuweze kuja kuzisimamia vizuri. Kwahiyo, mimi naungana na yale ambayo aliyozungumza naamini Mhe. Waziri baadae atakuja kutupa ufafanuzi kwa kuokoa muda mimi nilikuwa nataka niende tu kwa mambo ya jumla jumla.

Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa ndio tunaokaa tukapitisha bajeti, na katika bajeti tunayopitisha wananchi wanakuwa na matumaini makubwa sana kwamba zile fedha zilizoidhinishwa hasa katika taasisi mbali mbali, fedha zile zitakwenda kutumika kama vile ambavyo ilivyokusudiwa. Lakini kwa bahati mbaya sana tumeshuhudia katika kipindi cha zaidi karibu ya miaka mitatu au minne inakuja bajeti tunaidhinisha fedha muda unamalizika fedha zile hazikutumika. Sasa tunakuwa tunatengeneza manambari lakini manambari yale yanashindwa kuweza kufanya kazi. Na naendelea tena kutoa mfano kwa jambo ambalo halipendezi sana kwamba linarejeshwa kila mwaka hapa Barazani hasa katika masuala ya ulipaji wa fidia.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kuzungumza jambo ambalo bado siridhiki nalo ingawa kamati yangu ndio inasimamia suala zima la ukamilishwaji wa ujenzi wa barabara ya Wete/Chakechake. Barabara ambayo tokea mwaka 2009 inaingia katika vitabu vyetu tunaondoka tunapitisha bajeti tutalipwa *compensation* tunatenga katika bajeti zetu, lakini fidia ile inakuwa hailipwi. Fidia ile inaposhindwa kulipwa mnaipa tabu sana Wizara ya Mawasiliano pale wakati wa kutaka kuja kujenga barabara ile. Na huu nimeutoa mfano mmoja lakini nakusudia na barabara nyengine ambazo tayari zimeshakusudiwa kujengwa na tayari fedha zake za fidia tunakuwa tumeshazitenga lakini zinakuwa hazilipwi.

Matokezeo yake pale tunapotaka kujenga wafanyakazi wetu wa Idara ya Ujenzi au makampuni mbalimbali wanapata tabu, wanatukanwa na watu mbali mbali kwa sababu aidha kutokana na muda wa tathmini uliofanywa muda unakuwa ushakuwa mrefu, thamani ya malipo ya fedha zao wananchi wanakuwa wanaziona ndogo. Matokezeo yake tunasokotana na watu wetu, kwamba mradi wa maendeleo lakini unasababisha wananchi kulalamika. Sasa mimi kitu ambacho ninachokiomba bajeti ya mwaka jana tuliidhinisha fedha za *compensation*, bajeti ya mwaka huu tumeidhinisha fedha za *compensation*. Naomba sana hasa Wizara ya Fedha na Mipango mimi naamini fedha zile zingekuwa ziko Wizara ya Mawasiliano moja kwa moja basi fidia ile ingelikuwa tayari imeshalipwa. Lakini fedha zinabakia Wizara ya Fedha, Wizara ya Mawasiliano kazi yake yeye ni utekelezaji tu.

Sasa hili linatupa shida kweli kweli na Mhe. Mwenyekiti wewe mwenyewe shahidi humu humu ndani tulifika pahala tunasokotana na waheshimiwa katika masuala haya haya, nyumba inafanyiwa tathmini halafu pesa inayokuja kulipwa inaonekana ndogo thamani ya nyumba kwa wakati ule inakuwa kubwa. Sasa ndio maana ikawa nasema kwa kuwa fedha tayari tumeshaidhinisha kuna tatizo gani fedha hizo zisiende kulipwa. Nakuomba sana Mhe. Waziri wa

Fedha, waziri makini ambaye unasimamia majukumu yako vizuri hebu tunaomba suala hili lisijireje rejee ili hii bajeti tuliyoipitisha iwe *actual budget* sio bajeti ambayo pamoja na kwamba bajeti yetu ni *cash budget* lakini tuna matumaini kwamba pesa zinapatikana lakini zinashindwa kulipwa kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, sio hilo tu hapa Mhe. Waziri katika maeneo aliyotuomba, ametuomba maeneo matatu. Ametuomba tumruhusu akusanye lakini vile vile ametuomba tumruhusu katika hayo makusanyo kuna fedha za kodi, kuna fedha zile ambazo hazina kodi lakini vile vile kuna ile misaada pamoja na mikopo ya nje pamoja na ya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi zote tayari kupitia mswada huu tutamuidhinishia, lakini tatizo linalojitokeza kwamba katika zile fedha za malipo tunaambiwa kuna madeni ya nje na madeni ya ndani. Mhe. Mwenyekiti, kitu cha kusikitisha leo katika wizara zetu inafika pahala wizara inakopa tena inakopa kwa wafanyabiashara binafsi inachukua bajeti nne au tano ma-*suppliers* wale wanakuwa hawalipwi. Sasa je, hii tuliyoidhinisha fedha za kulipa madeni ya ndani, fedha hizi kwa nini zinakuwa hazitumiki kwa ajili ya kulipa madeni ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni nilipokuwa nikichangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha nilizungumza wazi wazi kwamba katika eneo ambalo kuna tatizo moja kubwa na hili naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa washirikiane kwa karibu sana Idara Maalum zimekopa sana, na zimekopa sana kwa wananchi wetu, wananchi wetu wanakata leseni, wananchi wetu kila siku *ZRB*, sisemi kwamba wanawasumbua wanafata kwa ajili ya kulipa zile kodi za serikali. Lakini serikali hiyo hiyo kupitia taasisi zake wanachukua vifaa wanakaanavyo zaidi ya miaka minne. Sasa hii bajeti ambayo tumeipitisha katika zile fedha ambazo za kulipa madeni ya ndani, yale madeni ya nje tunajua kuna utaratibu wa serikali kuna mikataba. Lakini haya madeni ya ndani Mhe. Mwenyekiti wakati bajeti hii tunaipitisha kwa nini fedha hizi zinakuwa hazilipwi kwa muda mrefu. Kwahiyo, Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema mwanzo mswada huu sio mkubwa, huu *just* kuidhinisha tu yale ambayo tuliyoyapitisha, lakini hiki tunachokiidhinisha tunataka kitumike kama vile maelezo yalivyojielezea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakushukuru sana baada ya kujibiwa hoja za Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa ukamilifu kwa mujibu wa taratibu zetu nitakuwa sina tatizo na kupitisha mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma, kwanza niwaombe wajumbe wote ambao wako nje ya ukumbi warudi ndani, na waliopo wasiweze kutoka waweze kufanya jambo hili mpaka limalizike. Nawaomba sana wajumbe ambao wako nje ya ukumbi warudi ndani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe waliopata fursa ya kuchangia Mswada wa Sheria ambao nimeuwasilisha, na waliochangia ni.

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa
2. Mhe. Ali Suleiman Ali na
3. Mhe. Hamza Hassan Juma

Kwanza alilolizungumza Mhe. Miraji Khamis Mussa alizungumzia kifungu cha 5(1) anasema kwamba Waziri anapewa karibu *blank cheque*. Ni kwamba aidhinishe uwezo huo ukitumika vibaya kama nimemfahamu vizuri ni uwezo ambao hauna kikomo. Sasa ninachotaka kumjuilisha tu Mhe. Mwakilishi akikisoma vizuri kifungu cha 5(1) kuna ukomo kwamba waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha anaweza kukopa wakati wowote ule, lakini sio zaidi ya tarehe 30 June, 2018 ikiwa ndani au nje ya Zanzibar kiasi chochote cha fedha ambacho hakitozidi kiasi kilichokubalika au kusemekana kukubalika kutoka mfuko mkuu wa serikali. Kwahiyo, kuna ukomo ndani ya hii bajeti ambayo tunaipitisha hapa waziri anaweza kukopa ndani ya ukomo ulioidhinishwa hapa. Kwahivyo, kuna *ceiling* hawezi kuamua tu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile Mhe. Miraji alizungumzia suala la ziada ya fedha. Nataka nimueleze tu na hii alizungumzia nadhani kwenye kifungu cha 6(1) dhamana ya waziri kutoa fedha zaidi, na hiki nimueleze kwamba kinaendana kwa mujibu wa kifungu cha 106 cha katiba ambacho akikisoma vizuri kina vifungu (a na b) ambavyo vinaruhusu kuwa na *supplementary budget.* Na huu utaratibu Mhe. Mwenyekiti umekuwa ukifanyika kila mwaka kwa utaratibu huu huu, kwa hiyo kuna utaratibu wa *supplementary budget* lakini vile vile kuna suala zima la kwamba waziri anaruhusiwa kuhamisha fedha kutoka fungu moja kwenda fungu jengine kwa maana ya *virement* ruhusa hiyo ipo.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile mawaziri wa sekta wanaohusika na wao katika kufanya uhaulishaji ndani ya vifungu vyao kwa mujibu wa sheria ya fedha. Kwahivyo, haya mambo yote anayoyaona hapa yapo kwa mujibu wa taratibu za kikatiba na sheria ambazo tumekuwa tukizitumia kwa miaka yote. Lakini pia kunapotokea hayo sasa ukienda kwenye kifungu ch 6(2) kinaelekeza haja ya kutaka kwamba taarifa iletwe katika Baraza hili. Sasa ukiwa na *supplementary budget* kuna utaratibu maalum wa kuwasilisha taarifa katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kuna suala jengine ambalo linawekewa tahadhari ikiwa kuna suala zima la dharura. Sasa hili suala la dharura huwa hatuwezi kulipangia kwa sababu sisi hatulijui sisi binadamu na likatokea hilo wakati sio kikao cha Baraza inabidi lazima apewe uwezo waziri anayehusika na masuala ya fedha kuikabili dharura hiyo, lakini baadae aje atoe maelezo katika Baraza kwa mujibu wa taratibu wa kishera zilizopo. Kwahiyo, mimi ningemuomba sana Mhe. Miraji akakubaliana na hoja tuliyowasilisha hapa haina matatizo ni utaratibu wa kawaida unaofuatwa na upo kwa mujibu wa katiba na upo kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la *figures* hili nimwambie tu kwa sababu ya haraka haraka hii tutaziangalia *figure* hizi baina ya ile kitabu kikubwa lakini pia na sheria hii, hili tutalifanyia kazi Mhe. Mwenyekiti na naamini halitokuwa kikwazo kwa yeye kutukubalia kufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na suala lake la kukasimu kwamba nadhani ilikuwa ni 6(3) ambayo inasema waziri mwenye dhamana na mambo ya fedha anaweza kukasimu uwezo wake alionao chini ya kifungu hiki. Kwahivyo, kinachokasimiwa sio majukumu ya waziri yote kwa ujumla wake, hapana. Kinachokasimiwa hapa ni kwa mujibu wa kifungu hiki cha sheria ambayo tunaipitisha. Kwahivyo, lile jukumu la waziri la kumshauri Rais liko pale pale, ningemuomba mheshimiwa akafahamu hivyo kwamba sikasimu kila kitu, lakini tunakasimu hii kwa ajili ya

kuweka utaratibu mzuri sana wa utekelezaji, na kinakwenda kwa mujibu wa masharti ya sheria iliyowekwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma yeye alizungumzia kuhusiana na fedha ambazo zinatengwa na kwa bahati huwa fedha hizo hazipatikani katika mwaka husika na alizungumzia masuala ya fidia ikiwemo fidia za barabara. Niseme tu kwamba kutofikiwa kwa bajeti iliyotengwa kuna sababu nyingi. Wakati mwengine hatufikii kwa sababu fedha zilizokusudiwa zitekeleze mradi huo kutoka kwa wafadhili hazikupatikana. Na kama fedha hizo hazikupatikana sasa na ile *counterpart fund* huwa haitoki. Kwahiyo, unaweza usifikie matumizi hayo kwasababu hiyo, lakini chengine ambacho kinaweza kutokezea ikawa pengine ule mradi wenyewe haujawa tayari kuanza kutekelezwa. Na tatu inawezekana kwa sababu tunatumia *cash budget system*, inawezekana makusanyo yetu yasitosheleze na kuna matumizi mengine ya lazima kwa hivyo kuna baadhi ya vifungu huwa vinakosa fedha hizo.

Kwa hayo yanatokezea na yanatokezea kwa dharura mbali mbali kama ulivyozieleza, lakini nimwambie tu kwa mwaka huu tunaomalizia na kama nilivyosema jana kwamba tumejitahidi sana. Na mimi naamini katika mwaka wa fedha 2017/2018 tunakusudia kuja na utaratibu mzuri zaidi ambao utahakikisha fedha zote ambazo zimepangwa katika bajeti hii ziweze kupatikana ili wizara ziweze kutekeleza majukumu yake. Hilo tunaliandaa na *Insha-Allah* Mwenyezi Mungu atatusaidia lakini kama nilivyosema sote tutekeleze wajibu wetu wale wanaotakiwa kulipa kodi walipe kodi, wananchi nao wawe wahamasishwe ili mapato ya serikali yapatikane na tuweze kuweza kuziendesha bajeti zetu hizi bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali yeye alitoa busara zake na naomba niseme tu kwamba ushauri wake tunaupokea na tutauzingatia. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hujatoa hoja, naomba utoe hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji sasa kama tumekubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wale wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya mwaka 2017

Kifungu 1 Jina fupi
Kifungu 2 Tafsiri
Kifungu 3 Utoaji wa Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Thamanini na Saba, Milioni Mia Tatu Hamsini na Tisa na Laki Nne kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali
Kifungu 4 Makisio ya Fedha zilizokubalika
Kifungu 5 Uwezo wa Waziri Kukopa
Kifungu 6 Uwezo wa Waziri wa Maombi ya Ziada

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nilimsikiliza kwa makini Mhe. Waziri alipokuwa akijibu akanipeleka kwenye kifungu cha 106 na pia nimekipitia kwa umakini sana; lakini maelezo yaliyokuwepo hapa alinijibu kuwa kuna dharura ambazo zinaweza zikatokea ambazo nazo pia zina sheria yake ambayo kwenye matumizi huko tumetunga sheria ambayo inaruhusu uwepo wa *emergency procurement* sawa katika kukamilisha, lakini hapa hakukuainishwa hiyo dharura ambayo Baraza haliwezi kukutana, hapa kilichokua kina mantiki kuonekana tunaikimbia ile dhana ya *supplementary budget* ndio maana ya kifungu hiki mimi kukikataa.

Sasa angeelezea tu katika matumizi ya dharura maana yake inajulikana dharura tukikubaliana hivyo waziri ninaweza nikampa mamlaka haya, lakini yale ambayo yamezungumzwa kifungu cha 106 kwenye kupokea zile *supplementary budget* zije na ziende na utaratibu kama Baraza ambalo limepewa majukumu kwenye kifungu cha 88 cha katiba kwenye maeneo yale mawili (a) na (b), ambayo tunapitisha mpango na tunapitisha bajeti kwa maana ya kujadili. Naomba maelezo ya ziada Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nikisome hiki kifungu kwa makini halafu na Mhe. Miraji Khamis Mussa atakisikiliza. Kwamba, "Uwezo wa Waziri wa maombi ya ziada, waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha ikiwa ataona ina manufaa kwa taifa. Kwanza hilo aliangalie. "Kutoa matumizi ya ziada kwa wizara au idara yoyote ya serikali ikiwa ni ziada ya fedha zilizokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa au kwa madhumuni ya huduma nyengine yoyote na itakuwa ni hasara kwa taifa kusubiri mpaka pale zitakapotolewa tena na Baraza la Wawakilishi".

Kwa tafsiri ambayo mimi ninayo na nafikiri na Mhe. Mwanasheria Mkuu anaweza kunisaidia, ni kwamba hapa kwanza halizungumzwi nje ya bajeti ile ya serikali ambayo imeshaidhinishwa ukiliangalia. Hii inatoa nguvu kwa sababu hata ukitizama bajeti ya mwaka 2016/2017 ziko wizara ambazo zimeongezewa zaidi ya kile kilichoidhinishwa na kutokana na dharura ambazo zinatokea. Kwa hivyo, uwezo huko anapewa waziri mwenye dhamana ya fedha ikiwa kutakuwa kuna haja ya kufanya hivyo na kwa manufaa ya taifa. Kwa hiyo, kuna wizara utazikuta zimepata asilimia 145 kinyume na vile ilivyopitishwa hapa, lakini kwa sababu ya dharura na umuhimu na kwa manufaa ya taifa.

Sasa huo ndio uwezo uliopo hapa, lakini kuna uwezo huo huo wa kufanya virement kutoka kwenye fungu moja kupeleka kwenye fungu jengine ikionekana kuna haja ya kufanya hivyo. Lakini waziri mwenye sekta na yeye kwa mujibu wa sheria ya fedha za umma ana haki ya

kuhaulisha ndani ya vifungu vyake na hili ni jambo ambalo nasema siku zote linafanyika, linatokezea na tahadhari hizi zinawekwa kwa sababu katika kupanga sisi tunaopanga ni binadamu hujui yatakayotokezea huko mbele. Kwa hiyo, kunakuwepo na dharura hizi ili zikitokea basi tusikwame na shughuli zetu kwa kusubiri kuja kukaa katika Baraza hili na taarifa zinatolewa na hata mara hii tumetoa taarifa tumewasilisha kwa zile sekta ambazo zimezidi matumizi. Sasa tena sijui Mhe. Miraji.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tafsiri aliyoieleza waziri inaanza kuingia akilini, lakini fursa na yale maelezo ambayo amesema kuwa tunachokijadili ni Bajeti Kuu ya Serikali ambayo kama labda kuna eneo moja wenzetu wamemaliza ile bajeti yao tunaweza tukawapa fungu jengine mimi sina tatizo. Lakini tatizo nililonalo kuwa pale ambapo imetokezea sio ile dharura lakini kutokezea kwa matumizi ambayo hata ule mpango wake hatujaupitisha, ndio tatizo nililokuwanalo.

Mhe. Waziri, lakini akikiri kuwa haya yote kwa mujibu wa kifungu hiki yataendana na mpango tulioupitisha kwa zile kesi za kawaida, lakini kwa kesi za dharura sina tatizo, akiri hapo tu, kuwa kifungu hiki tukimpitishia yeye atakiendesha kwa mujibu wa zile fedha tu ambazo tumepitisha mpango wake wa maendeleo. Lakini kwa kesi ya dharura haina mpango wa maendeleo tunajua, tusije tukapokea yale matumizi huku mbele ambayo hata ule mpango hatukuupitisha lakini pia si dharura, ndio kesi ambayo mimi nilikuwa nataka nimnyime fursa waziri kwa eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia katika eneo hilo hilo kwa sababu ndio nimesimama kabisa, kwa sababu hiyo 6 ina vifungu 1 mpaka 3.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa kwanza tumalize hili la kwanza, upate jawabu hili moja kwanza halafu utakuja na hilo la pili.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Sawa Mwenyekiti, nimekukubalia kwa sababu hicho kifungu Nam. 6(1) kina 6(3) pia, kwa hivyo usije ukaninyima kifungu cha 6(3) ukaondoka hapo.

Mhe. Wazri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri Mhe. Miraji ameshanielewa, naamini kabisa ndugu yangu huyu ameshanielewa. Lakini kwa faida yake pengine na Baraza kwa jumla nirudie kusema kwamba, Kifungu hiki cha 6(1) kinazungumzia ziada ile itakayotokea katika mahitaji ya wizara au idara, ambayo hii nimeshaisemea itasaidiwa sana na kufanya uhaulishaji kwa maana ya *virement* ya kutoka fungu moja kwenda fungu jengine. Hili limo ndani ya bajeti hii ambayo imeshapitishwa na wakati mwengine kunatokea dharura ambazo zinasaidiwa na Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini ndani ya bajeti ambayo ilithibitishwa na siyo nje, ikitokezea kwamba matumizi sasa ni zaidi ya hiki kilichopitishwa hapa kuna utaratibu wake, utaratibu wa kuja na *supplementary budget* ambao uko wazi kabisa. Sasa Mheshimiwa naomba kwa hili atukubalie kwamba taarifa na maelezo yetu ni hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis nadhani umeshafahamu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu hayo ya waziri maana yake keshaelekea kukiri kuwa yale mengine atakuja nayo kwenye *supplementary budget* peke yake,

hansard zipo na tukija kukutana mbele ya safari *Insha-Allah*. Lakini kifungu cha 6(3) sasa ambacho nilisema kuna 6(1) na (3), hiki nimeshamkubalia lakini kikipitishwa maana yake kimepitishwa moja kwa moja kwa hiyo, niseme hiki kabisa.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea,

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tena, nilitoa mawazo yangu kwenye kifungu cha 6(3) ambapo Mhe. Waziri kwenye majibu yake, mana hata mimi nilikataa kabisa kumkasimisha awe na uwezo wa kumkasimisha afisa yeyote, na mantiki yangu kwa waziri katika jukumu lake nilisema la kumsaidia Rais na kumshauri; ndio majukumu mawili makubwa ya msingi ambayo yamo ndani ya katiba ya nchi yetu. Sasa anapokuja kumkasimisha afisa yeyote na yeye alisema katika majibu yake, naomba kidogo tu Mwenyekiti, kwa muda wako niyanukuu. Alisema: "Namkasimisha kwa mujibu wa haya mambo yaliyokuwepo hapa", maana kile kitendo tu cha waziri kumkasimisha afisa yeyote kufanya kazi ni dhambi kwa mujibu wa Katiba. Kwa sababu yeye Katiba ya nchi imempa mamlaka ya moja kwa moja na kayalia kiapo na alipokula kiapo hakusema kuna siku nitamkasimisha, hebu anipe tena tafsiri ya ziada kidogo kipi ambacho kinamruhusu yeye bila ya kutenguka kwa Katiba hii.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, nilichojaribu kueleza wakati nikitoa ufafanuzi ni kwamba kifungu hiki hakimaanishi kwamba waziri mwenye dhamana ya fedha anakasimisha majukumu yake ya uwaziri. Haikukusudiwa hivyo, lakini katika uendeshaji wa bajeti; bajeti hii inaendeshwa na inaendeshwa wakati mwengine kwa msaada wa watendaji na mtendaji mkuu katika uendeshaji wa bajeti hii ni Katibu Mkuu ambaye yeye ni *Pay Master General.* Kwa maana hiyo, hata tulipopitisha fungu la Wizara ya Fedha Katibu Mkuu huyu hatukumpa dhamana ya kusimamia fungu lile, fungu lile sasa linasimamiwa na Naibu Katibu Mkuu.

Kwa hivyo, hapa tunazungumzia *issue*s za *operation* na ndio maana tukasema kukasimisha huku ni kwa mujibu wa kifungu hiki cha 6 na ni *delegation* ya yale majukumu yangu, lakini pia yataambatana na masharti kwa mujibu wa sheria, kwamba hapewi tu akakasimiwa yote, lakini kile unachomkasimu basi kinaendana na masharti ambayo waziri mwenye dhamana ile ndiye atakaeyatoa masharti.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo cha kusema ile dhamana na jukumu la yote yatakayotokezea bado yanabebwa na waziri husika, waziri mwenyewe mwenye dhamana ya fedha. Kwa hiyo, bado jukumu liko pale pale na kama suala la kumshauri Mhe. Rais bado waziri mwenye dhamana ya fedha anamshauri Rais katika masuala yanohusiana na fedha kwa mujibu wa matakwa ya katiba na sheria.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji nadhani umeridhika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Hapana, Mhe. Mwenyekiti, si mkaidi katika kuisaidia serikali lakini na kuwasaidia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hii dhana nzima. Mimi kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa maelezo yake, lakini nataka akubaliane na mimi

alimtolea mfano Katibu Mkuu ambaye hata yeye anakula kiapo kwa Mhe. Rais kwa majukumu yake na ile wizara, maana yake majukumu yake yanaonekana wazi huyo Katibu Mkuu wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikamwambia aniweke wazi anataka kumkaimisha nini maana ya kumkasimisha nini ambacho kiko nje ya sheria ambayo yeye Katibu Mkuu kaapa lakini na yeye kiko nje ya utaratibu ambao Mhe. Waziri kaapa, hawa wote wawili. Mana tuwachukulie mfano huyu huyu aliyemtolea yeye na ndio maana nikasema hiyo *operation* aliyoisema Katibu Mkuu tayari ana *operation* pale alipo, ndio maana hata wizara yake kwa sababu ana *operation* ya Mfuko Mkuu wa Serikali pakawa na naibu ambaye ataiendesha Wizara ya Fedha.

Sasa naelewa yote Mhe. Mwenyekiti, lakini aniweke wazi akiacha kiapo alichoapa Katibu Mkuu katika kazi zake na kazi zake yeye, hiki anachotaka kumkaimisha na hapa imeandikwa afisa yeyote kwa nini maelezo yake haya yanaelekea huko tusiseme tukamkasimisha tukawataja tu Katibu Mkuu, ikisha hao wengine wote tukawafuta mana afisa yeyote anaweza kumkaimisha hata Kamishna, hata Mkurugenzi tu, kitu ambacho ndio kinatupa mashaka.

Wizara ya Fedha hii ngumu, yeye mwenyewe anajua kuna madhambi tele hapa anakuja kuyasema pesa zimetolewa katika mtandao, kumtaja yule ambaye alikuwa afisa mas-ula wa kipindi kile pia hakuweza kumtaja. Mheshimiwa nataka majibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nimemsikia Mhe. Miraji Khamis Mussa, lakini nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri ambayo ameifanya ya kutoa ufafanuzi kwenye vifungu ambavyo vimeulizwa.

Kwanza Mhe. Miraji Khamis Mussa akitaka kusoma kifungu hiki vizuri na apate tafsiri ile ambayo imekusudiwa angesoma kwanza kifungu cha 2 cha sheria hii, mengi ya maneno ambayo humu hayakutafsiriwa maana yake tafsiri imeachwa kwenye Sheria ya Fedha, ile sheria ndio inayoongoza tafasiri ya maneno mengi ambayo yametajwa ndani ya sheria hii na huyo afisa ambaye hakutajwa humu maana yake sheria ya fedha tayari imeshamtafsiri ni afisa gani ambaye amepewa dhamana ya kushughulikia mambo haya ya fedha.

Sasa kwa humu kwasababu haikutajwa tafsiri hiyo lazima kwanza asome ile sheria yenyewe ya fedha na uzuri wake kama tumeibadilisha kuna sheria mpya sasa ya matumizi ya fedha za umma ndio imetoa tafsiri kubwa ya maneno haya. Lakini ukiisoma ile sheria kuna kazi pia ambazo Mhe. Waziri amepewa ndani ya ile sheria, ambapo ukiisoma ile pamoja na hii ndio Mhe. Waziri sasa amepewa fursa na sheria hii kukasimu baadhi ya kazi zake kwa afisa na afisa kwa mujibu wa sheria ya fedha ni afisa mas-uli ambaye ndiye anakuwa afisa dhamana wa mambo ya fedha.

Kwakweli, ile sheria mpya ukiisoma kuna majukumu maalum ya waziri yametajwa na kuna majukumu maalum ya Katibu Mkuu ambayo yametajwa. Lakini humu kifungu hicho ukikisoma kinasema waziri anaweza, maana yake hiki hakimlazimishi waziri kutoa madaraka yake lakini akiyatoa basi ayatoe kwa masharti maalum. Kwa sababu dhamana bado inabaki kwake yeye, yeye ndiye waziri ambaye kwa mujibu wa sheria ndio anachukua hiyo dhamana. Sasa nimuombe Mhe. Miraji Khamis angesoma na ile sheria ya fedha vizuri akaifahamu angeyajua majukumu ya waziri ambayo yameelezwa nini ndani ya ile sheria na majukumu ya afisa *mas-uli* yameelezwa

nini, halafu akajua kile ambacho kinataka kukasimiwa kwa mujibu wa vifungu hivyo. Nakushukuru Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa muda wako ushamaliza kwasababu hoja hii umeshanyanyuka zaidi ya mara tatu na nyongeza mara moja. Kwahivyo, kwa mujibu wa kanuni inabidi tuendelee.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa kifungu hiki ndio nainuka mara hii ya tatu na ndio ya mwisho.

Mhe Mwenyekiti: Kifungu ndio hiki hiki Nam. 6 hii itakuwa ni mara ya tano.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Hii ndio mara ya tatu ya mwisho nikimaliza hapa tunakwenda katika huo utaratibu unaonielekeza.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba tuendelee kwasababu hili limeshatolewa maelezo sana, Mwanasheria Mkuu pia ameshalitolea maelezo, Waziri wa Fedha na Mipango ameshalitolea maelezo na zaidi ametoa ufafanuzi Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa kanuni itabidi tuendelee. Mhe. Waziri.

UTARATIBU

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nimesema kunako kifungu hiki cha 6(3) mimi ndio mara yangu ya tatu kutaka kusema na nasema ndio mara yangu ya mwisho. Lakini ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa haya yote ni kifungu cha 6, kwa hivyo yote yaliyohusiana ni kifungu kimoja.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ndio pale mwanzo nilizungumza mapema kuwa huku kuna hoja mbili na aliyonijibu ni moja na wewe ndio uliruhusu.

Mhe. Mwenyekiti: Umeshatoa hoja zaidi ya nne, nakuomba tuendelee Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Basi mimi sikuridhika na majibu haya kwasababu nilikuwa nataka kufika pahala nitoe maelekezo, maana Mwanasheria Mkuu hapa tumemruhusu kasema lakini hicho kifungu cha sheria mama yeye ndiye Mwanasheria alisaidie Baraza hili mbona kashindwa kukitaja kainuka tu. Maana Mwanasheria kwenye Baraza hili akaanza kufanya siasa si wajibu ambao unamleta humu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Naomba Mhe. Miraji Khamis Mussa tuendelee. Katibu tunaendelea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelekeza yeye ili apate kuchangia vizuri na nimemtajia sheria ili wakati mwengine akija akaisoma hiyo sheria, mimi sio *cyclopaedia* kama sheria zote za nchi hii zimo kichwani mwangu, hata na mimi pia nafanya *reference*, sio

kwasababu Mwanasheria Mkuu basi ndio sheria zote za nchi hii zimo kwenye kichwa changu. Hata mimi natakiwa nifanye *reference* na ndio maana nikamtajia sheria ya fedha ambayo tumeipitisha juzi ambayo imefuta sheria ya mwaka 2005, akaisome ili aje kuchangia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Katibu tunaendelea.

Kifungu 6 Uwezo wa waziri wa maombi ya ziada
Kifungu 7 Marejesho ya mkopo na riba
Kifungu 8 Kukubaliwa kwa mipango ya maendeleo
Kifungu 9 Kukubaliwa kwa fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendeleo

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali bila ya marekebisho. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha wanyanyuwe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Makisio ya Matumizi ya Mwaka 2017

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya mwaka 2017 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Makisio ya Matumizi ya mwaka 2017 ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kupitisha mswada huo. Sasa katibu tunaendelea.

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake anazoendelea kutujaalia katika nchi yetu na kwa neema hizo ndio sote tumeweza kukutana tena leo hii na kuniwezesha mimi binafsi kusimama mbele ya Baraza hili kuwasilisha Mswada wa Sheria Fedha ya mwaka 2017.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa utaratibu wetu kuwasilishwa mswada huu ....

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, bado kazi tunaendelea. Kwahivyo, Waheshimiwa Wajumbe mubaki katika sehemu zenu. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa utaratibu wetu kuwasilishwa mswada huu kunaashiria kukamika kwa mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha na kuidhinishwa kwake na Baraza lako tukufu.

Naomba nikupongeze wewe binafsi Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Spika, Naibu Spika, pamoja na Mwenyekiti mwenzako wa Baraza kwa jinsi unavyoliongoza kwa ufanisi Baraza letu hili katika kikao chetu cha sita cha Baraza hili la tisa ambacho kinaendelea na kina muelekezo wa kumalizika kwa mafanikio makubwa.

Aidha namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. Mohammed Said Mohammed, namshukuru sana pia Makamu wake Mhe. Bahati Khamis Kombo na Waheshimiwa Wajumbe wote wa kamati hiyo kwa uweledi waliouonesha katika kujadili mapendekezo ya mswada huu na ushauri wao uliopelekea marekebisho kadhaa katika mswada ninaouwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ya Fedha kutokana na mapitio ya kila mwaka yanayofanywa na serikali katika mfumo wake wa kodi. Sheria nyengine zinazohusiana na mapato na inabidi sheria nyengine kufanyiwa marekebisho muhimu. Mapitio hayo hubainisha maeneo yanayohitaji kuwekewa sheria mpya, kuimairishwa na hata kasoro zinazohitaji kuondoshwa katika baadhi ya sheria zetu.

Sheria ya fedha kutumika kufanya marekebisho kwa sheria mbali mbali kama inavyohitajika. Huu ni utaratibu wa kawaida unaotumika katika nchi nyingi duniani na pia tunautumia hapa Zanzibar.

Madhumuni, Mhe. Mwenyekiti, mswada unaowasilishwa una madhumuni yafuatayo:-

(1) Kurekebisha sheria zilizotajwa ili kuwa na sheria zitakazowezesha ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi zaidi.

(2) Kurahisha zaidi ukusanyaji wa kodi kwa kutumia teknolojia ya kisasa na simu za mikononi pia na uwazi zaidi katika maeneo mbalimbali.

(3) Kuimarisha usalama kwa malipo ya mishahara kuingizwa moja kwa moja katika hesabu za watumishi katika Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

(4) Kuimarisha udhibiti wa karafuu na kuzuia usafirishaji wake kwa njia ya magendo.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2017 umegawika katika sehemu 7.

Sehemu ya masuala na utangulizi na sehemu sita zilizobaki ni kulingana na sheria zilizopendekezwa kurekebishwa na ziko kama ifuatavyo.

Sehemu ya kwanza ni maelezo ya awali yanayohusu jina na kutumika kwa sheria.

Sehemu ya pili inawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya usimamizi na utaratibu wa kodi namba 7 ya mwaka 2009. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga katika kuweka utaratibu wa matumizi wa vifaa vya kodi na simu za mikononi katika ulipaji na ukusanyaji wa kodi na mapato mengine ya serikali. Marekebisho yanaimarisha uwazi katika kushughulikia makosa kwa kwa kuweka utaratibu wa kufuatwa na kamishna katika kutoa hati ya makosa. Marekebisho hayo pia yanalenga katika kudhibiti mifumo maalum ya kujipatia nafuu ya kodi isivyo halali.

Mhe. Mwenyekkiti, sehemu ya tatu inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *VAT* namba 4 ya mwaka 1998. Kimsingi marekebisho yamedhamiria kuhalalisha utozaji wa *VAT* unaofanywa na benki kwa kuzingatia marekebisho yalifanywa mwaka 2016 katika Sheria ya *VAT* ya Tanzania Bara. Kwa vile benki zinatumia mifumo sawa baina ya Tanzania Bara na Zanzibar zimeendelea pia kukusanya kodi hiyo kwa Zanzibar bila ya kuwasilisha serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya 4 inapendekeza marekebisho madogo katika Sheria ya Ada za Petroli Namba 7 ya mwaka 2001, kwa kuweka tafsiri sahihi ya mafuta yaliyosafishwa (*refined petroleum product*). Lengo ni kuwa na utaratibu wa kisheria wa utozaji wa kodi kwa mafuta hayo pale yanapoingizwa kwama malighafi na kusafishwa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya tano, inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Karafuu Namba 2 ya mwaka 2004. Mapendekezo yanahusisha uingizaji wa vifungu vipya 5 kwa madhumuni ya kusimamia magendo ya karafuu ikiwemo upigaji marufuku magendo ya karafuu, uingizaji wa karafuu na utoaji wa siri za usimamizi wa magendo. Marekebisho pia yanalenga kuweka hatua za kuchukuliwa ikiwemo za kutaifisha au utaifishaji wa karafuu miche na makonyo.

Sehemu ya 6 Mhe. Mwenyekiti, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kazi Namba 11 ya mwaka 2005 kwa kuweka sharti kuwa mishahara yote katika ajira rasmi ilipwe kwa kupitia benki.

Sehemu ya 7 Mhe. Mwenyekiti, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mafunzo ya Amali namba 8 ya mwaka 2006 ya kuondoa gharama za mafunzo na sare za kazi katika pato la mfanyakazi linalotumika kwa madhumuni ya kutoza ushuru wa kuendeleza ujuzi (*skill development levy)***.**

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waujadili mswada huu na hatimaye kuupitisha mswada huu ili uwe Sheria ya Fedha ya mwaka 2017.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aweze kuleta hotuba yake Mhe. Mwenyekiti, karibu. Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti endelea.

Mhe. Asha Abdalla Mussa (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti naomba kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na kurekebisha baadhi ya sheria za fedha na kodi kuhusiana na ukusanyaji wa udhibiti wa mapato ya serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani za awali nazitanguliza kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma kwa kuendelea kutukarimu neema zake zisizo na kifani. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, ili kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na kurekebisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi, kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii isingeweza kukamilika bila ya mashirikiano makubwa waliyonipatia Wajumbe wa Kamati yangu katika kuupitia mswada huu. Hivyo, kwa dhati kabisa napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano wao ambao umepelekea zoezi la kupitia mswada huu kukamilika kwa ufanisi mkubwa. Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo;-

1. Mhe. Mohammed Said Mohammed — Mwenyekiti
2. Mhe. Bahati Khamis Kombo — Makamu Mwenyekiti

3. Mhe. Abdalla Ali Kombo Mjumbe
4. Mhe. Zulfa Mmaka Omar Mjumbe
5. Mhe. Asha Abdalla Mussa Mjumbe
6. Mhe. Shehe Hamad Mattar Mjumbe
7. Mhe. Simai Mohammed Said Mjumbe

Aidha, napenda kuwatambua na kuwashukuru makatibu wa Kamati yangu ambao ni;

8. Ndg. Abdalla Ali Shauri Katibu
9. Ndg. Kassim Tafana Kassim Katibu

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya mswada huu ni kufanya marekebisho katika baadhi ya sheria zinazosimamia ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo, ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa sheria hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza serikali kwa kuwasilisha mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu, ambao utasaidia kuongeza ufanisi na udhibiti mzuri wa mapato pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi, biashara na teknolojia inayotokea duniani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, serikali imedhamiria kutoongeza kodi yoyote mpya. Hatahivyo, pamoja na kutokuwepo kwa ongezeko la kodi kwa upande wa Zanzibar, inawezekana kabisa mabadiliko ya kodi yatakayofanywa upande wa pili wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yakaathiri Zanzibar. Hivyo, kamati yangu inaishauri serikali kuzingatia jambo hilo kwa umakini mkubwa kutokana na namna linavyoweza kuleta changamoto kwa wafanyabiashara na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla, sambamba na kutafuta namna bora ya kukabiliana na changamoto hiyo, iwapo itajitokeza, ili dhamira na malengo ya Serikali ya kuwapunguzia mzigo wananchi yaweze kutimia.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unafanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi ikiwemo Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya 2009, ambapo miongoni mwa marekebisho ya msingi yanayofanywa ni kuweka masharti ya matumizi ya "Mashine za Kielektroniki" kwa kutoa stakabadhi kwa malipo ya bidhaa au huduma zinazotolewa. Kamati yangu imepata imani kuwa, sasa serikali imedhamiria kutumia mfumo wa kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato, kwani kutotumika kwa mashine hizo imekuwa ni kilio cha muda mrefu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako, ambao tunaamini mfumo huo kwa kiasi kikubwa utapunguza mwanya wa uvujaji wa mapato ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inashauri matumizi ya mashine za *"EFDs"* yaanze kwa taasisi za serikali kabla kutumika katika sekta binafsi, ikiwemo bandarini pamoja na maeneo yote yanayohusika na mapato ya utalii. Hili litasaidia kuhamasisha wananchi katika kuzitumia mashine hizo kwa kuona ufanisi wake na pia kukubali kulipa kodi kwa hiari. Sambamba na hilo, kamati yangu inashauri suala la elimu lipewe kipaumbele katika kuwafahamisha wananchi kuhusu umuhimu na wajibu wa kuzitumia mashine hizo.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuepuka utata wa utekelezaji wa sheria hii, kamati yangu pia inashauri yaekwe maelekezo kwenye kanuni, ambayo yataweka wazi utaratibu utakaotumika kwa maeneo ambayo hakuna huduma ya umeme au pale ambapo huduma ya umeme itakosekana.

Mapendekezo ya Marekebisho ya Mswada

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu iliupitia mswada huu na kuibua marekebisho mbalimbali, baadhi ya marekebisho hayo ni pamoja na marekebisho ya kisarufi ambapo vifungu mbalimbali vimerekebishwa ili kuvifanya visomeke vizuri na vilete maana iliyokusudiwa, baadhi ya vifungu hivyo ni kifungu cha 7 cha kinachorekebisha kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, ambapo neno ***"fiscal"*** liliopo baina ya neno " neno" na neno **"**baina**"** linapendekezwa lisomeke **"**kielektroniki**"**

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati yangu ni kuweka usawa wa maneno baina ya Mswada wa Kiswahili na Mswada wa Kiingereza ili Miswada hii iendane, na kuleta maana halisi iliyokusudiwa. Mfano wa vifungu vilivyorekebishwa ni kifungu cha 8 cha Mswada ambacho kinarekebisha kifungu cha 22A cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, kwa kuongeza neno "kutunza**"** baina ya neno "kupokea**"** na neno **"**kutuma**".**

Mhe. Mwenyekiti, Marekebisho mengine yaliyopendekezwa na kamati yangu ni kufuta baadhi ya maneo ambayo yanaonekana hayaleti maana yoyote katika vifungu hivyo, mfano wa maneno hayo ni katika kifungu cha 3 cha Mswada kinachorekebisha kifungu cha 3 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, mbapo neno "*za*" liliopo baina neno "*maalum*" na neno "*zinatumika"* linapendekezwa kufutwa. Aidha, katika kifungu cha 16 cha Mswada maneno "Sheria ya**"** yaliopo baina ya maneno "sheria ya**"** na neno **"**kodi**"** yanapendekezwa kufutwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia, ilifanya marekebisho yanayotokana na makosa ya kiuchapaji kwa lengo la kuweka bayana usahihi wa maneno hayo. Katika kifungu cha 17 kinachorekebisha kifungu cha 2 cha Sheria ya Kodi Ongezeko la Thamani Nam 4 ya 1998, katika aya ya (e) neno **"**utowaji" liliopo baina ya neno **"**inayohusisha**"** na neno **"**au**"** lnapendekezwa lisomeke **"**utoaji**".** Aidha, katika aya ya "g" neno "kiwangoi**"** liliopo baina ya neno **"**au" na "chengine**"** linapendekezwa lisomeke " kiwango**"**

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni baadhi tu ya mapendekezo ya marekebisho yaliyofanywa na Kamati yangu, naamini Waheshimiwa Wajumbe wamepatiwa waraka wa Kamati unaonesha mapendekezo yote ya marekebisho ya huu ambayo Kamati yangu imeyapendekeza.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya kamati kuhusu mswada huu. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba wajumbe wa Baraza lako hili, wauchangie, waujadili, na hatimae kuupitisha mswada huu, kwa lengo la kukuza ufanisi, na udhibiti wa mapato ambao utapelekea kuongezeka kwa mapato ya nchi yetu kwa taasisi zilizopewa jukumu la kukusanya mapato**.**

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha. Nakushukur. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Asha Abdalla Mussa. Waheshimiwa Wajumbe, hoja iko mbele yetu kwa hivyo tunaweza kujadili. Mhe. Hamza Hassan Juma, endelea.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe Mwenyekiti, nataka nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri, lakini vilevile nitakazia maoni ya kamati ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa mara nyengine tena nataka nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ni mtu msikivu sana kwasababu yeye alipoingia katika wizara hii alitukuta hapa Barazani tunalalamika. Tulikuwa tunalalamika kitu kikubwa mapato ya serikali kupotea au kuvuja, na tulikuwa tuna ushauri mwingi sana tulikuwa tukijaribu kuutoa siku za nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika eneo ambalo tulikuwa tukililalamikia sana ni fedha za serikali kukusanywa halafu zikatiwa mkobani. Mkoba kama tunavyoujua, mkoba kwa kweli kuhifadhi fedha zinaweza zikafika pahala msizione, na kuna mifano mingi. Katika kipindi cha nyuma ilikuwa viwanja vya kufurahisishia watoto, tulikwenda mimi na kamati yangu Pemba kule tukamkuta yule muhusika anamkoba wa ukili, tukamuuliza hizi fedha ukishazikusanya unafanya nini. Kwasababu kwanza tulimuuliza unaziweka wapi. Akasema naziweka mkobani na mkoba wenyewe ndio huu, na kweli tulizikuta. Sasa halafu unazifanya nini. Akasema halafu nazigawa mafungu matatu, fungu moja nawapa wafanyakazi hapa, fungu jengine sijui napeleka wizarani na fungu jengine sijui, yaani anakusanya anatia kwenye mkoba halafu anagawa mafungu kama tungule. Kwa kweli tukaona daa! kumbe ndio maana hivi viwanja vyetu vinajengwa na serikali, lakini baada ya muda mchache unakuta viwanja vimechakaa wakati fedha zinakusanywa.

Lakini pia hata Uwanja wa Ndege wetu wa *Zanzibar International Airport*. Mhe. Mwenyekiti, pale palikuwa na yale malipo ya *VISA* ya wageni, na pale tulipiga kelele sana karibu bajeti tatu tulikuwa tunapiga kelele, jamani mapato ya *VISA* Uwanja wa Ndege wa Zanzibar yanapotea, pale wanakwenda wako ambao wanalipa lakini wako wengine ambao hawalipi. Lakini matokezeo yake tukaja tukafanya hesabu kuna kipindi Mhe. Mwenyekiti, tukauliza makusanya ya *VISA* pale Uwanja Ndege, tukaambiwa walikuwa wanakusanya kwa mwaka ilikuwa ni karibu milioni 300 mpaka milioni 500.

Lakini baada ya kupiga kelele sana wakapewa ile kazi wenzetu Benki ya *CRDB*, wakaambiwa wakae pale wawe mawakala wa *ZRB* kwa ajili ya kuweza kukusanya mapato ya *VISA*. Mhe. Mwenyekiti, kitu cha kushangaza, pesa ambazo zilikuwa zikikusanywa shilingi milioni 500 kwa mwaka, Mhe. Mwenyekiti, pale zilikusanywa karibu shilingi bilioni 3.5 kwa miezi 9. Sasa angalia kutoka milioni 500 mpaka bilioni 3 ndani ya miezi 9.

Mhe. Mwenyekiti, tukaendelea kuishauri serikali, wale wenzetu wa *CRDB* walishauri mambo mengi. Walishauri kwamba zile fedha wanaokusanya pale *Airport* waruhusiwe wakusanye na maeneo mengine, wakajaribu kutoa ushauri kama maeneo ya *Beit-el-Ajaib* kule, yale maeneo mengine ambayo katika sehemu za utalii. Lakini vile vile wakapendekeza mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika mahoteli yetu mbalimbali.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aendelee kushirikiana na wenzetu wa *CRDB,* ili waweze kutukusanyia mapato kama inavyotakiwa. Sasa angalia mapato yaliongezeka kwa asilimia karibu 500 ndani ya miezi 9, mapato yalikusanywa kwa zaidi ya asilimia 500, sasa tuone mapato ya serikali yanavyopotea.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, jitihada za Mhe. Waziri tumeziona, tulikuwa hata masuala ya leseni haya tulikuwa sisi tunakwenda tunalipa *cash* pale, na pale unapokwenda kulipa *cash* unaona hasa ule utaratibu wa hifadhi ya zile fedha zilikuwa hazionekani. Lakini sasa hivi utaratibu umeanzishwa fedha zinakusanywa benki, sasa hivi tumeona mapato ya serikali yamekua kwa asilimia kubwa sana.

Kwahivyo Mhe. Mwenyekiti, siku zote tunasema bado kuna mapato ya serikali hayajakusanywa na kama yatakusanywa mapato ya serikali tulikuwa tunazungumza, tuna uwezo wa kwenda bajeti yetu tukakusanya mpaka trilioni moja. Nashukuru kwamba bajeti ya mwaka huu tunategemea tutakusanya karibu fedha trilioni 1.08. Kwahivyo, Mhe. Mwenyekiti, hii inaonesha kama serikali itasimamia mapato yake vizuri, basi bajeti yetu tutakusanya fedha nzuri, nyingi na fedha zile zitakusanywa halafu zitatumiwa kwa maslahi ya wananchi.

Tumeona Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu. Mimi ndio maana nikasema bajeti ya matumaini, kwa sababu zile fedha zote ambazo zilizoongezeka katika makusanyo ya bajeti ya mwaka huu Mhe. Mwenyekiti, zimeelekezwa moja kwa moja katika ile mikakati maalum ambayo inakwenda moja kwa moja katika kuboresha hali za maisha yetu, pamoja na miundombinu ya maeneo yetu mbali mbali.

Kwahivyo, mimi kitu ambacho nakipongeza katika mswada huu zaidi katika kile kifungu kinachozungumzia kwamba sasa hivi tayari tuna halalisha sheria ya yale mapato yanayokusanywa kwa kupitia simu zetu za mikononi. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi ukiangalia makampuni ya simu yanakusanya fedha nyingi sana, lakini makampuni yale ilikuwa hakuna utaratibu wa kurejesha kodi serikalini.

Sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru na hivi juzi nilimsikia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango tulipomuuliza, akasema kwamba katika utaratibu wa sasa hivi ile mikato tunayokatwa katika simu za mikono tunapofanya *transaction* za fedha, fedha zile ile kasma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inakwenda moja kwa moja *ZRB* kwenda katika Hazina ya Zanzibar. Sasa hii kwa kuwa na sisi tulikuwa tunahitaji tuwe na nguvu ya kisheria. Tunashukuru Mhe. Mwenyekiti, katika mswada huu imeelezewa kwamba sasa hivi sheria itakuwa inasimamia zaidi katika suala zima la hizi fedha za siku za mikononi.

Vilevile Mhe. Mwenyekiti, utaratibu ambao Mhe. Waziri aliokuja nao katika sheria hii, kwamba sasa hivi ile mishahara ndio yale yale tunayozungumza, mambo ya mtu tena kwenda kupewa pesa mkobani sasa hivi yaondoke. Nafikiri sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, mishahara moja kwa moja ikipitia benki mimi nafikiri itakuwa kila kitu *transaction* zinaonekana na mishahara ikipitia benki Mhe. Mwenyekiti, hata lile suala zima la mishahara hewa litaondoka, kwa sababu benki kama huna kitambulisho, kama sio mfanyakazi halali huwezi pale ukenda ukatoa pesa. Kwa hivyo, sheria hii ya mswada huu Mhe. Mwenyekiti, naamini tukishaupitisha, ndio ile ahadi na mapendekezo ya Mhe. Waziri kukusanya fedha zaidi tunategemea tutaweza kupata.

Lakini, nije katika hoja ambayo Mhe. Waziri ameelezea kwamba inakusudia kudhibiti masuala mazima ya zao la karafuu. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ukiangalia katika taarifa mbalimbali za serikali, karibu miaka mitatu nyuma Pemba peke yake zilinunuliwa karafuu karibu za shilingi bilioni 70. Mhe. Mwenyekiti, hiyo pesa sio ndogo ni pesa nyingi kweli kweli. Lakini tujiulize pesa ile ilikuwa inakusanywa mkobani hakuna kodi ya serikali. Kwa hivyo, tunaamini fedha ile kama ingekuwa inapitia katika *process* za kawaida inalipwa kwa kupitia benki, lakini vile vile kwa utaratibu ambao serikali inakuja nao, basi tunaamini mapato yataweza kupatikana yataweza kuboresha miundombinu hasa katika barabara za vijijini kule Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, tunaamini sana kwamba utaratibu huu ambao aliokuja nao Mhe. Waziri utaweza kusaidia sana kuongeza mapato yetu. Pia kodi za mabenki ni kweli mabenki yanafanya *transaction* kubwa sana, sisi tunatuma fedha nje, lakini vile vile tunapokea fedha nje na pia tunafanya *transaction* ya fedha za mabenki kwa kupitia *account* za mabenki mbalimbali. Tunategemea Mhe. Mwenyekiti, sheria hii tukishaipitisha itasaidia sana kuweza kuongeza mapato yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa kamati mimi kwa kweli naunga mkono kwa asilimia mia moja. Hizi mashine za *EFD* zianzie ndani ya taasisi zetu za serikali. Mhe. Mwenyekiti, mapato ya serikali yanapovuja ndio pale bajeti zetu zinatikisika. Kwahivyo, kabla ya kuanza kuzipeleka kwa wafanyabiashara, mimi nadhani kama walivyosema wenzangu tuangalie, kwanza tuanze na wafanyabiashara wakubwa, lakini zijazwe katika taasisi zetu za serikali, halafu baadaye zisambae mpaka vijijini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vijiji humu kuna watu wanatengeneza pesa nzuri sana, kuna biashara kubwa sana. Leo Mhe. Mwenyekiti, lakini hakuna kodi ya serikali inayopatikana, ukiangalia maeneo ya fukwe mbali mbali, ukienda Kiwengwa, Nungwi, ukienda Kwendwa kule kuna biashara nyingi kubwa sana, tena biashara nyengine Mhe. Mwenyekiti, zinaendeshwa kwa malipo ya dola moja kwa moja, lakini serikali haina chochote ambacho inakusanya pale. Kwa hivyo, hizi mashine za *EFD* kama nilivyosema Mhe. Waziri juzi au sijui jana tulimuuliza katika semina na walituahidi kwamba hizi mashine za *EFD* zipo nyingi, tena za kisasa zitaweza kukusanywa katika maeneo mbali mbali.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo ambayo nilikuwa nataka Mhe. Waziri ayaangalie ili kuweza kuongeza mapato ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tunazungumza sana kuhusu suala zima la hizi nyumba bubu, maana yake kuna *guest bubu* na nyumba bubu vitu viwili tofauti. *Guest bubu* ni ile ambayo watu wanaingia na kutoka, lakini nyumba bubu Mhe.

Mwenyekiti, watu wanaingia wanaweza wakaa mwezi mzima, wengine wanaweza wakakaa miezi miwili au miezi mitatu tofauti na *guest*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi ulimwengu tunaokwenda nao ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Namuomba sana Mhe. Waziri tunajua watu wa Uhamiaji kwa kushirikiana na watu wake wa *ZRB*, wanakwenda kuangalia katika zile nyumba ambazo zinakodishwa na serikali haipati mapato. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kama nilivyosema teknolojia ya sasa hivi imekuwa sana, kuna nyumba ukitaka kwenda nchi yoyote, wewe unataka kukodi nyumba wala huna haja ya kwenda kumtafuta papasi, unaingia tu kwenye mtandano Mhe. Mwenyekiti. Naomba sana Mhe. Waziri hebu fungua mtandao halafu uangalie *Airbnb*, hapo utazikuta hizo nyumba nilizokuambia zote za Zanzibar ambazo zinakaliwa na wageni ambapo serikali haipati kodi utaziona hapo, ingia kwenye *Internet* ukifungua tu utaziona zilizokuwepo Paje, utaziona zilizokuwepo Uroa, utaziona zilizokuwepo Mjimkongwe na kila pahala, hayo mapato bado hatujayakusanya Mhe. Mwenyekiti. Kwahivyo, katika eneo hilo mimi naamini tunaweza kukusanya kodi nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile nilikuwa nataka niseme kwamba iko haja na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumepata semina ndogo, lakini semina ile kwa uzito ambao tulioichukulia, iko haja sasa hivi tuanze kushuka kwa wananchi wetu katika vikao vyetu mbali mbali, kwenye mikutano yetu mbali mbali tuwafahamishe wananchi wetu umuhimu wa kuja kutumia hizi *EFD machine*.

Mhe. Mwenyekiti, tunasafiri nchi mbalimbali, unakwenda kununua ile penseli, huwezi kwenda dukani kununua penseli Mhe. Mwenyekiti, ukapewa tu penseli ni lazima unapewa na risiti, unakwenda kununua pini, ile pini ya kufungia shati, unakwenda kununua *office pin* lazima unapewa risiti yako. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kupitia hizi mashine za *EFD* kwakweli zitaweza kutusaidia sana kukusanya mapato na kuongeza mapato ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sikwenda moja kwa moja katika vifungu, lakini nilitafsiri vifungu jinsi gani ambavyo vitakavyoleta tija kwa nchi yetu na kuongeza mapato ya serikali. Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, namuunga mkono Mhe. Waziri. Lakini vile vile naunga mkono hotuba ya kamati ya bajeti. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma. Sasa namwita Mhe. Miraji. Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, naona Mhe. Miraji Khamis amekukaa kidogo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia mswada huu muhimu sana wa sheria ya kutoza kodi. Lakini pamoja na kukushukuru wewe nichukuwe fursa hii vile vile kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwa kuleta mswada huu muhimu sana ambao una lengo la kuweza kuhakikisha kwamba ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali unakwenda vizuri na hatimaye kupelekea ufanisi zaidi katika utekelezaji wa sheria hizo mbalimbali, ili kuona kwamba serikali inapiga hatua katika suala zima la kuongeza mapato yake na hapo ndipo uchumi wetu utaweza

kuimarika. Vilevile, niishukuru Kamati ya Bajeti kwa uwasilishaji wao kuhusiana na mswada huu. Nimpongeze sana mjumbe aliyenitangulia Mhe. Hamza Hassan kwa uchanganuzi wa kina wa mchango.

Mhe. Mwenyekiti, nije moja kwa moja sasa na mimi niweze kutoa michango yangu kidogo kuhusiana na mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, mswada huu kutokana na nilivyoupitia nimeona kwamba unakusanya sheria mbali mbali na kuzifanyia marekebisho. Kwa ghafla nimeziona kuna sheria karibu sita. Kuna Sheria ya Usimamizi wa Kodi namba 7 ya mwaka 2009, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani namba 4 ya mwaka 1998, Sheria ya Kodi ya Mafuta namba 7 ya mwaka 2001, kuna Mswada wa Maendeleo ya Karafuu namba 2 ya mwaka 2014, kuna Sheria ya Ajira namba 11 ya mwaka 2005, vilevile kuna Sheria ya Mafunzo ya Amali namba 8 ya mwaka 2006.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu kama nilivyosema una marekebisho ya sheria karibu sita. Sheria ambazo zimetajwa nyengine au nyingi zao tayari zilikuwa zimeandikwa kwa lugha ya Kingereza, inakuwa ni vigumu sana kwa muda mfupi, kwasababu kama unataka uutendee haki huu mswada basi ni vyema kuweza kuzipitia sheria hizo sita ili uweze kuona yale mapungufu ambayo yalijitokeza na nini ambacho kinarekebishwa. Kwahivyo, naliomba sana Baraza hili, kwanza hizi sheria ambazo ni za zamani na ambazo zimeandikwa kwa lugha ya Kingereza, nafikiri umefika wakati kuweza kuzitafsiri kwa lugha ya Kiswahili.

Vilevile Mhe. Mwenyekiti, mswada ya namna hii ambayo ina marekebisho ya sheria nyingi mbalimbali, ni vyema ipatikane mwanzo ili mjumbe aweze kujiridhisha kuweza kutazama sheria ambazo zimetajwa ndani ya mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 15 kwenye kifungu cha 9(23)(2), hapa kuna maelezo napenda niyanukuu.

> "Bila ya kujali masharti ya kifungu (1) Kamishna anaweza kumsamehe mtu au kikundi cha watu kutoa stakabadhi ya malipo ya kielekroniki au ankara za kielektroniki kwa kutumia mashine za kielektroniki".

Mhe. Mwenyekiti, wasiwasi wangu uko katika misingi ya kusamehe mtu, naona iainishwe, kwa sababu kama hakuna misingi haijaainishwa aidha katika sheria au kanuni, inawezekana pengine kamishna huyu akaweza kuja ku-*take advantage* na kuweza kuja kujipendelea, sasa hapo kutakuwa kuna mgongano wa kimaslahi. Kwahivyo, aidha kuwe na kanuni ambayo itaeleza misingi ya kusamehe. Aidha, ndani ya sheria hii basi misingi hii iwe wazi ili kuepusha baadhi ya watu kuja kusamehewa lakini kutokana na *interest* za kamishna huyu.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika ukurasa wa 16 Mhe. Mwenyekiti kulikuwa na suala zima la utoaji huu katika kifungu cha sita cha juu hapa ambacho kinasema,

> "Stakabadhi ya kawaida ya malipo mauzo au Ankara ya kodi zitachapishwa kwa mtiririko wa nambari na kwamba hakuna nambari itakayotolewa zaidi ya mara moja".

Mhe. Mwenyekiti kipengele hichi ni kizuri sana nakipongeza kiendelee kubaki lakini lazima tujue kwamba kuna wafanyabiashara, ambao wanaweza wakawa wanachapisha risiti zao au ankara zao kwa njia ya *store*, inawezekana mkupuo huu ameweza kutolesha vitabu 100 vya risiti na akaanza na nambari moja mpaka nambari iliyofikiwa lakini vikimaliza vile anachapisha vyengine anaanza tena na namba moja. Sasa utakuja kukuta kwamba hizi namba moja zinakuwa ziko mbili sasa hapa lazima kuwe na utaratibu mzuri, vilevile wa kuwasimamia wale wafanyabiashara ambao wana mtindo huu, lakini vyenginevyo kuna uwezekano mkubwa wa nambari hizi za risiti kujirudia kwa mujibu wa mfanyabiashara jinsi gani utaratibu wake wa kuchapisha hizi ankara au risiti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee ukurasa wa 20 katika suala zima la kifungu cha 19(a) hapo suala zima la kupiga marufuku magendo ya karafuu. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi ambacho kina vifungu vidogo vidogo vingi kifungu kidogo 2 ambacho nacho kina kifungu (a) na (b) hapa kuna hoja kwamba napenda ninukuu kwanza.

> "Ikiwa mtu atatiwa hatiani chini ya kifungu kidogo cha 1(a) cha kifungu hichi atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka saba na kisichozidi miaka 15 na wakati anatumikia adhabu yake atapanda miche 70 ya karafuu".

Mhe. Mwenyekiti, kwanza hapa isomeke miche 70 sio ya karafuu miche 70 ya mikarafuu, baada ya marekebisho hayo tujiulize kwanza utekelezaji wa adhabu hii ya kupanda miche 70 akiwa yuko gerezani. Mimi ninavyojua kwamba gereza lina mkusanyiko wa wahalifu watenda makosa mbalimbali, kwahivyo watakuwemo pamoja na hawa ambao wamehusika na suala hili la mambo ya karafuu. Sasa sijui itaenda *order* gani gerezani juu ya mfungwa ambaye amewekwa kwa kosa la magendo ya karafuu, ili kuweza kutekeleza adhabu hii ya kupanda mikarafuu, au miche ya mikarafuu 70. Kwakweli, naona hii adhabu haijanikalia vizuri halafu kuna wafungwa inawezekana wako mijini na sasa vilevile tatizo jengine haikuwainishwa atapanda katika mashamba gani, katika mashamba ya serikali au mashamba ya watu binafsi.

Lakini nani atakuwa anafanya *follow up* ya kuhakikisha kwamba mfungwa yule kabla hajatoka ameweza kupanda hiyo miche 70. Kwahivyo, hichi kifungu kama hakina ulazima basi tukiondoshe ibaki tu adhabu pengine ya kifungo cha miaka fulani au kama kuna adhabu ya faini basi kibaki hicho, kwasababu tusiweke kifungu ambacho utekelezaji wake kwakweli hatuuoni kama utakuwa una ufuatiliaji na nina ushahidi wa kutosha, kwamba leo Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inatoa miche ya mikarafuu bure lakini nimepata jibu hapa hakuna *follow up* inayofanyika juu ya wale tunaowapa seuze huyu mfungwa ambaye tunasema aje apande miche 70 hii nafikiri tunajidanganya. Hivyo, kama haina ulazima basi hii adhabu hii tuiondoshe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika kifungu cha 19(c) naipongeza sana serikali ni marufuku kwa mtu yeyote kuingiza karafuu Zanzibar kwa madhumuni ya biashara. Kwakweli, niipongeze sana serikali kwa kuweka kifungu hicho ni ukweli usiofichika na nilisema hapa katika bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi vilevile kwamba kuna wanjanja wachache ambao hivi sasa wanachukua karafuu nje ya Zanzibar na kuziingiza Zanzibar.

Kwahivyo, nashukuru sana serikali kuliona hili kwasababu tungefikia pahala basi ile *brand* yetu ya karafuu yetu nje ikaanza kudharaulika kwasababu ingeweza kuchanganywa karafuu zetu za Zanzibar na karafuu zinazolimwa katika mikoa ya Morogoro, Tanga na hii ingeweza kushusha soko letu la karafuu ulimwenguni. Kutokana na hali hiyo, naishukuru sana serikali kwa kuweza kuliona hili na hili litaweza kutusaidia ili karafuu yetu iweze kuwa na hadhi ile ile ambao tunayo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika ukurasa wa 12 pana kifungu kidogo cha 3 juu hapo ambacho kinasema " Endapo mtu atatiwa hatiyani kwa kosa chini ya kifungu hiki Mahakama pamoja na adhabu iliyotolewa itatoa amri kwa mtu huyo kulipa serikalini kiasi cha fedha sawa na kilichopatikana kutokana na mauzo ya karafuu zilizotaifishwa".

Hapa Mhe. Mwenyekiti, napendekeza naona iko wazi hii adhabu kwa mfano kimetaifishwa pangine kipolo kimoja cha karafuu maana yake kwa nilivyofahamu kitapigwa thamani, ili uweze kulipa, lakini sasa hawa ni wahujumu wa uchumi iwe ni kipolo kimoja au iwe ni magunia 100 mimi nafikiri iwekwe adhabu ya fedha kulingana hasa na uzito ili watu wasiweze kuingia katika hatua hii ya magendo ya karafuu. Kama tunaweka milioni kumi au milioni tano na hadi hapa nafikiri ingekaa vizuri zaidi kuliko hivyo ilivyokaa kwamba aweze kutoa hizo fedha kwa mujibu wa usawa wa kile ambacho amekamatwa nacho, nafikiri wengi wanaweza kuichezea hii sheria.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije sehemu ya 6 ukurasa huo huo kwenye marekebisho hapo nafikiria kuna neno limeachwa kwa hivyo napendekeza liingie hilo neno kwenye kichwa cha habari hapo, marekebisho ya ya ajira nafikiri palikuwa na neno limekuwa *missed* hapo marekebisho ya Sheria ya Ajira Nam. 11 isomeke hivyo napendekeza.

Lakini nikija katika ukurasa wa 23 katika sehemu ya saba kifungu cha 33 ambapo neno la pembeni linasomeka "*construction"*. Nisingependa hilo neno la Kingereza kwasababu huu Mswada ni wa Kiswahili liondoke ili liwekwe neno muafaka na lenye maudhui na muktadha wa *construction.* Kwakweli, sina mapendekezo hapa kwasababu ni lugha ya kisheria kidogo. Kwahivyo, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu basi atoe tafsiri hapo ili hilo neno liweze kubakia .

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi niupongeze sana mswada huu umekuja wakati muafaka ambao utaifanya serikali yetu kuweza kudhibiti na kukusanya mapato, ili kuweza kwamba uchumi wetu unapiga hatua na tunaondokana na utegemezi. Hivyo, Mhe. Mwenyekiti niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe na wao waupitie na hatimae wauchangie na tuweze kuunga mkono. Kwahivyo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia kwa mia juu ya mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa namwita Mhe. Zulfa Mmaka Omar kuendelea na kutoa mchango wake.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kutia baraka zangu katika mswada huu. Kwanza nianze na pongezi za dhati kwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa jitihada zake zote anazoifanya kwa kubana mapato yetu yasiibiwe na yasipotee na tuyatumie katika njia iliyo nzuri. Pia nimpongeze Mhe. Rais kwa

kumteua Waziri wa Fedha huyu Dkt. Khalid hapa niseme kwamba kafanikiwa kwa asilimia mia moja hii kazi anaiweza, anaifanya inavyotakiwa na nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi zake, ambazo anazifanya na tumwambie kwamba asiogope lawama za watu waibaji katika nchi hii tunachokitaka sisi ni maendeleo ya nchi sio maendeleo ya mtu mmoja mmoja ambaye haipendelei Zanzibar yetu na Tanzania kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niipongeze tena serikali hii kwa juhudi zake wanazozichukua kwa mashirikiano na mawaziri wote katika kuwabana watendaji wetu, ili wasiweze kuzichukua pesa hizi za nchi na kuzitumia kwa mambo yao ambayo wanayataka. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano tumemuona Mhe. Waziri kipindi cha nyuma tu ambapo kawabanda sana watendaji na sasa hivi watendaji wale ambao walikuwa na majumba kumi kumi sasa hivi kwakweli hali yao imekuwa mbaya kidogo, kwasababu wizi katika serikali hii sasa hivi hauna nafasi na wao tunawaona kwamba ni njia gani wanaumia, hapa kuna baadhi ya watendaji ambao wako katika ukusanyaji wa pesa hizi tunawashuhudia kwamba unamkuta mtu mlinzi tu katika wizara fulani ana majumba kumi ukimuliza kwakweli pesa zile zinatoka wapi ni dhahiri unakuta kwamba lile ni jizi la serikali. Kwahivyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuwabana hawa watu na nimwambie kwamba ashike uzi huo huo na sisi tutamsaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika ukusanyaji huu nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuona kwamba ipo haja pesa hizi kukusaywa kwa njia ya kibenki tunaona kwamba sasa hivi mapato yote ambayo unataka kwenda kulipa tukiangalia kama *ZRB* kuna ambao wanakwenda kulipa mchanga, ambao wanakwenda kulipa mawasiliano wanakwenda pale kulipa. Lakini nimuombe Mhe. Waziri watu wale wanakwenda kulipa pale katika *PBZ* zetu, lakini tunaona kwamba wakati wa kwenda kulipa wanapata usumbufu mkubwa wa kukaa foleni, unamkuta mtu anakwenda kulipa shilingi elfu tatu tu lakini anakaa foleni masaa manne hofu yangu mimi wasije kuona kwamba pesa ile wanataka kuilipia lakini wakakimbia ile adha ya kukaa foleni muda mkubwa sana na kukimbia kutokulipa pesa zile naamini kwamba na wao watasumbuka, lakini na serikali pia itakakosa mapato yale ambayo tunayategemea.

Kwahivyo, nikuombe sana Mhe. Waziri suala hili ni zuri na sisi tunalipenda ila sasa uangalie ni njia gani itatusaidia kuondoa msongamano ule wa wananchi wanaokwenda kulipa mule mabenki ili kutokupoteza lile ambalo tumelikusudia, nishauri kwamba kama kuna uwezekano yafunguliwe matawi madogo madogo ambayo yatawezesha wananchi wale kulipa pesa zile kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende sehemu ya wananchi tunaona kwamba sasa hivi pato letu limezidi sana tuna juhudi kubwa sana ambazo tunazifanya mapato haya kuzidi. Lakini sasa kuna miradi Mhe. Mwenyekiti, ambayo inafanywa kutokana na pesa za wananchi, niseme kuna wananchi kwamba hawaelewi zile pesa ambazo zinakusanywa zinafanywa kitu gani na ukiangalia kwamba pesa zile ambazo tunazikusanya sisi zinafanya mambo makubwa sana katika nchi yetu. Kwahivyo, nimuombe tu Mhe. Waziri aendelee tena kutoa elimu ya juu kwa wananchi wetu, ili waondoke kusema kwamba pesa zile wanazikusanya lakini hakuna faida ambayo inafanywa, kwa sababu pesa hizi zinazokusanywa zinafanya mambo mengi sana tunapata madawa, tunapata barabara, tunapata umeme, tunapata kila kitu lakini sasa unakuta kwamba wananchi wetu elimu bado ni ndogo sana juu ya suala hili.

Kwahivyo, nikuombe sana Mhe. Waziri usisite kufanya vipindi katika maredio *TV* ili kuelewesha wananchi pesa hizi ni kitu gani tunafanyia ili na wao waone faida ya pesa ambazo tunazikusanya.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika Mashine za ki-*electronic* Mhe. Waziri nikupongeze sana kwa kuchukua juhudi hizi za kuleta mashine hizi naamini hapa pia ni njia ambayo utawazuia tena hawa majizi wa serikalini wasipate kuziiba hizi pesa za wakulima na wakwezi, tunaona kwamba mashine zile zitakapoletwa pesa hizi itakuwa ni ngumu sana kuchukulika tukiangalia wenzetu Tanzania Bara sasa hivi mashine zile wanazitumia na tunaona kwamba kuna faida yoyote ambayo inapatikana. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana kwa kuleta mswada huu naamini kwamba hapa napo pia patazidisha tena mapato yetu ya nchi kama ambavyo yamezidi na leo tunakupa pongezi za juu kwa kuidisha mapato haya. Kwahivyo, nikuombe sana itakapopita tu sheria hii tusisubiri kukaa sana ili vipato watu watumie mashine hizi na pato letu la nchi lizidi na wananchi wapate kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika suala la ukusanyaji pesa kwa mfano kama wale ambao wanatoa risiti feki, sasa hivi kuna watu wanatoa risiti feki utaikuta risiti ile juu imeandikwa pesa ambayo mimi nimeshawahi kuzikuta hasa kuna wizara juu wanaandika pesa kubwa lakini chini katika risiti ile unakuta kwamba kuna pesa ndogo ambayo wanaandika Mhe. Mwenyekiti pale wanaiba. Kwahivyo, nikuombe sana hizi risiti za kuandika kwa mkono Mhe. Mwenyekiti sasa hivi hazifai zifutwe kabisa kwasababu tunaona kwamba wanatumia risiti hizi kwa kufanya mambo yao, kwa mfano ukienda hospitali utaandika kipimo kitakuwa shilingi 2000 kwenye karatasi ya juu utaandikiwa shilingi 2000 lakini risiti chini ukija kuikagua utakuta kuna shilingi 500, kwakweli bado udanganyifu upo na nikuombe sana uzidi kufuatilia masuala haya na nikuombe sana sheria hii ipitishwe haraka, kwasababu tunaona kwamba kuna baadhi ya pesa bado zinaibiwa katika serikali yetu.

Kwa juhudi ambazo umekuwa nazo na imani ambayo umetuonyesha Mhe. Waziri, naamini kwamba suala hili utalifanya haraka iwezekanavyo na sisi tuko pamoja na wewe na tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie imani yako juu ya nchi hii na akuzidishie utendaji wako juu ya kuwabana hawa majizi katika serikali yetu hii na wafikie kiwango waseme sasa basi kuiba, kwa sababu Waziri aliyekuwepo hataki masihara wala hataki mchezo mchezo katika majukumu yake. Kwahivyo, nikupongeze sana na nimpongeze sana tena Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein nimwambie kwamba hapa kachagua jembe na sisi tupo pamoja na wewe bega kwa bega na nawaomba wananchi wenzangu tuiunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na tumpe baraka zote tumuamini kwamba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango suala hili atalifanya itakiwavyo.

Mhe. Mwenyekiti baada ya maneno hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Zulfa Mmaka Omar. Sasa namwita Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Balozi Amina Salum Ali kutoa mchango wake.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nichangie katika mswada huu wa serikali unaofanya marekebisho katika sehemu mbalimbali, pia niunge mkono yale mambo ambayo yamependekezwa kwatika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa ningeomba nizungumze kidogo kuhusu hii *EFD*. Mhe. Mwenyekiti naomba niunge mkono kifungu hichi cha kuanzishwa taratibu wa risiti za *Electronic* niseme tu kwamba wakati umefika na sisi Zanzibar kuingia katika utaratibu huo na kusema kweli tumechelewa kwa kweli, kwa sababu nchi nyingi za ukanda wetu huu wanatumia vifaa hivi. Kwahivyo, niwatoe wasiwasi wananchi wa Zanzibar kwa kusema kwamba utaratibu mzuri utafanywa wa kuwawezesha wafanye wanunue bidhaa zao bila ya usumbufu lakini vilevile serikali ipate taarifa za wafanyabiashara na taarifa za biashara zinazofanyika nchini lakini pia kulinda mapato ya taifa letu.

Kwahivyo, ninachosema tu kwamba sisi kama serikali tutaharakisha utaratibu huo kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na ikifika mwakani kama alivyosema mwaka huu katika kipindi tulichokuwa tumekubaliana utaratibu huu utaanzishwa ili tuweze kwenda katika usasa ambao unatakiwa. Kubwa ambalo ninaloliona wanalofanya wafanyabiashara hata kama wakati mwengine hiyo risiti ipo nchi za nje tunavyoona wanakwambia je, unataka kuchukua bila ya risisi au unataka kulipa risiti, ukisema nataka risiti yangu basi wanakwambia bei tofauti huo ndio ujanja wanaofanywa na wafanyabiashara.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kwamba wafanyabiashara kama walivyokuwa wako pamoja na serikali na serikali inawapa kila kipaumbele basi na wao waanze na wawe wawazi vilevile kwa ajili ya shughuli hii. Mhe. Mwenyekiti, vilevile naomba nije sasa marekebisho ya Sheria ya Karafuu hii imo katika ukurasa 20...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri subiri kidogo, Waheshimiwa Wajumbe ni karibuni tutapitisha vifungu hapa kwahivyo kama *quorum* haifikii tutakuwa tunachelewesha shughuli zetu naomba mlioko nje mfanye utaratibu wa kurudi Barazani. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko endelea.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti nawashukuru wenzangu wajumbe waliochangia marekebisho haya ya Sheria ya Maendeleo ya Karafuu Nam. 2 ya mwaka 2014. Nasema hivi Mhe. Mwenyekiti kwasababu lazima wote tunakubali kwamba umuhimu wa zao la karafuu ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Na wote tunajua historia ya zao la karafuu lilivyotoka tukaletewa Zanzibar tukalihudumia tukapata misukosuko mbalimbali tulikuwa juu tukizalisha mpaka tukateremka chini, mpaka tuko chini lakini sasa tunapanda juu kidogo kidogo, hiyo historia inaeleweka wote humu wajumbe wanaelewa na wananchi wanaelewa.

Lakini changamoto tunazozipata ni nyingi Mhe. Mwenyekiti. Changamoto ya kwanza huko nyuma kulikuwa na makelele mengi, kwamba watu wakitaka karafuu ibinafsishwe ili wananchi wawe wananunua, wanachuma karafuu zao wanauza karafuu zao wanavyotaka wenyewe. Lakini hilo serikali imeshasema mara nyingi Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein kila wakati anapokuwa anazungumzia maendeleo ya Zanzibar, hasa kunako zao la karafuu tunasema karafuu haibinafsishwi, kwasababu tunaona nchi nyengine huko ambao karafuu zimebinafsishwa hawapati fursa, hawapati kipaumbele kama tunapopatiwa kipaumbele hapa Zanzibar katika zao hili la karafuu.

Lakini, changamoto nyengine Mhe. Mwenyekiti ni kwamba karafuu za Zanzibar zinapigwa vita na magendo, magendo na hawa wanaofanya magendo ni wengi. Ikawa kuna utaratibu kuna *tax force* tunazoziweka, tuna wasimamizi mzuri lakini bado hawa wanadili wanaofanya mambo ya magendo wanatuumiza kwasababu karafuu zinapenya. Huko nyuma naomba niseme kwamba wakati katika sheria za zamani ukikosa kosa la karafuu la magendo au na mambo mengine yanayolingana na hayo kosa lake zamani ilikuwa kali sana. Zamani ukikutwa na karafuu magendo basi adhabu yake kifo lakini tumekwenda katika ustaarabu tuingia katika mambo ya utawala bora tumesema sasa hivi karafuu, tukasema adhabu ya kifo katika mambo hayo iondoshwe matokeo yake magendo watu wanafanya magendo bila kuwa na simanzi.

Na ukifanya magendo ni muhujumu uchumi, kwasababu asilimia zaidi ya 99 Wazanzibari wanategemea karafuu kama hujatumia karafuu kwenye mafuta ya kujitia mgogoni unaumwa basi unapiga mswaki, basi unatumia katika mambo mengine kwenye chakula basi lakini vile vile, hata kama vile ukifa Mhe. Mwenyekiti dalia inachanganywa na karafuu. Kwahivyo, sisi wote Wazanzibari tunatumia karafuu kuanzia kuwa mchanga mpaka unapokuwa unakwenda kaburini unatumia karafuu. Kwahiyo, mtu ambaye anaharibu karafuu kwa magendo huyo ni mtu ambaye anauhujumu uchumi, huyo ni muhujumu uchumi kwahiyo hatua kali kabisa zinatakiwa zichukuliwe na ndio maana serikali kwa makusudi ikakubali kufanya marekebisho hayo ya Sheria ya Maendeleo ya Karafuu, ili kutoa adhabu kali kwa yule ambaye anahujumu karafuu zetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti naomba nikinuu hiki kifungu kwasababu kuna wengine wanajidai kama hawafahamu, hawana fahamu hawafahamu hawataki kujua kwamba hili karafuu ni zao ambalo tunalitegemea. Juzi nikisoma gazeti kuna kikundi kinaitwa ubaya ubaya juzi nimesoma kwenye gazeti au jana huko Pemba kuna kikundi kinaitwa ubaya ubaya. Kwa maana kwamba hichi kikundi hakiogopi serikali wala hakiogopi wala hakina inami na wenyewe wenye mikarafuu yao, wanapita wakikata miti ya mikarafuu na wengine wengine wana majina na ajabu ajabu na wengine wao wanakuwa kama wale madoni katika mafia kuna mtu anamtandao mkali kabisa anasema yeye ni rais wa magendo. Ningeomba nichukuwe nafasi hii kumpa salamu huyo Rais wa magendo ya karafuu na mtandao wake kwamba serikali safari hii tumejiandaa zaidi, tena zaidi na tuko imara kabisa hapa tunamtambua Rais mmoja tu, Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein hatutabui Rais mwengine yoyote nchi hii. *(Makofi)*

Sasa kama kuna rais wa magendo wa karafuu basi nampelekea salamu wanasema watoto wa mijini tunam-*dip* kumwambia safari hii tutakula naye sahani moja. Lakini Mhe. Mwenyekiti wale ambao kama hawa ubaya ubaya umeshaanza kufanya mambo yao ubaya ubaya ya kukata miti ya mikarafuu, tunaomba kuwapa salamu na hawa pia kwa sheria hii tunawafunga watu bila ya kuona imani. Mhe. Mwenyekiti nasema hivyo kwa sababu kesi za magendo ya karafuu huko nyuma toka kuanzia mwaka 2014 mpaka leo kesi zile hazijahukumiwa, hatujawaona wahalifu waliohujumu mikarafuu hatujawaona wahalifu waliokata mikarafuu, hatujawaona wahalifu ambao wamekutwa na karafuu mijini kwasababu sheria ile ilikuwa sio kali sana, mpaka sasa hivi wanajisifu na wanatembea mjini na mpaka wamejiita majina kwamba wao ni marais na wao wenye mtandao mkali sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria hii Magendo maana yake nini wamesema, ni usafirishaji uchukuwaji usio halali katika chombo cha baharini, angani, nchi kavu au uhaulishaji au uondoshaji usio halali wa miche ya karafuu, karafuu yenyewe makonyo ya karafuu au bidhaa zinazotokana na karafuu kwa madhumuni ya kuzitowa sehemu moja kwenda sehemu nyengine ndani au nje ya Zanzibar, hii tafsiri imebana kitu chochote cha karafuu basi imebana kwahivyo ninachosema Mhe. Mwenyekiti wasijitie watu ubabaifu wakasema hawajafahamu. Kifungu hichi kiko wazi kabisa kinapiga maarufu karafuu au aina ya karafuu miche ya karafuu kama uko angani au nchi kavu ama baharini una karafuu ambapo sio sehemu ya kusafirisha karafuu unakamatwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini ikawa kifungu hichi kwasababu hapo nyuma kukiwa na karafuu Wete mfano au Chake Chake hata kama baada ya kazi usiku, unaambiwa wewe huna hujafanya magendo ya karafuu ndani ya gari hujafanya magendo karafuu. Karafuu mpaka uonekane baharini ndio kama wewe unaonekana kama una magendo ya karafuu kifungu hichi kinabana kwahiyo, watu wakae tu vizuri watatiwa hatiani watu wengi. Na wataiogopa karafuu kama wanavyoogopa moto vile au umeme. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana katika kusema kwamba karafuu sasa hivi zimetiwa hatia, mtu ana hatia, mtu anakuwa mkosa kwa kufanya vitendo ambavyo vimeorodheshwa katika vifungu hivi, lakini pia Mhe. Mwenyekiti nimefurahi sana katika kuangalia adhabu kama nilivyosema miaka yote hii, toka 2014 hatujasikia mtu aliyepewa adhabu kwasababu kwa sheria zile wakisema wenyewe walioko kule kunakohusika, kwamba sheria haziwapi nafasi wale majaji na wanaokamata kuwa siya kwenye adhabu.

Kwahiyo, safari hii visingizio hivi Mhe. Mwenyekiti havipo, tukiangalia kifungu 19(a) kifungu namba 27 lakini kifungu 19(a) Nam. 1 kwenye chenye (a) (b) (c) na (d) kinachoeleza mambo gani ambayo yatakufanya wewe uchukuliwe hatua. Kwa mfano, ukifanya magendo ya karafuu, miche ya mikarafuu, ukifanya magendo mhalifu lakini pia ukijaribu kufanya magendo mhalifu, lakini ukila njama ya kufanya magendo mhalifu vilevile ukishiriki pia mhalifu, kuna watu wameshiriki katika magendo ya karafuu watu wameshiriki tunajua kama hawa wameshiriki lakini huko nyuma ah! Sikushiriki anatolewa kesi inakuwa haipo, sheria hii inamfunga. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba wananchi wa Zanzibar na wenzangu wajumbe hapa mkawafahamisha wawafahamishe kunako mikarafuu, sheria hii inafunga. *(Makofi)*

Lakini pia kumetokea mtindo mmoja Mhe. Mwenyekiti na huu wakusafirisha miche ya mikarafuu, miche ya mikarafuu imekuwa mali kwa nini, imekuwa mali kwasababu serikali yetu inatowa miche mikarafuu bure, kwahiyo watu walivyokuwa watu wa Unguja hawajali hawathamini nguvu za serikali zetu wanachukuwa miche hiyo wanakwenda kuiuza Bara. Tanga, Morogoro kwa sheria maarufu atakae kamatwa na miche ya karafuu mbele huku kuna vifungu vya adhabu. Mhe. Mwenyekiti mimi naunga mkono sana sheria hii na nnaifurahia kama utaingia msimu mpya wa karafuu, tunaingia na hatua mjarabu kwamba wale wakorofi wanaotuharibia zao letu la karafuu huu ni muarubaini sana, dawa sana itakayofanya wale wote ambao wamejiandaa sasa hivi kwa magendo ya karafuu na kuharibu na kukata mikarafuu kuchoma mikafuu wamejiandaa basi hii itawakuta mahali pazuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa makosa nimefurahi sana kunako makosa hatia ambayo atakuwa anapewa mtu, kwanza yule ambaye anafanya magendo Mhe. Mwenyekiti imenifurahisha sana yule anayekuwa magendo kwamba yeye atakaa miaka saba jela, kati ya miaka saba na asizidi miaka 15 lakini jambo zuri ambalo nimelifurahia na niombe kumjibu Mhe. Mwenyekiti mmoja aliyezungumzia hili, kwamba atalazimika apande miche sabiini elfu ya karafuu aone nayeye uchungu wa kupanda mikarafuu hii miche sabiini elfu itakuwa miche yake aipande katika kipindi kile ambacho anatumikia Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, anaweza kwasababu kutoka vifungo kuna aina nyingi unaambiwa wewe utakwenda jela, utapigwa bakora, unaenda jela unapigwa na bakora upo huo utaratibu lakini pia unaambiwa unakwenda jela unafanya kitu fulani, kwa hiyo hapa tunasema utakaa jela lakini huko huko jela utapelekwa mashambani ukalime mikarafuu. Miche yako sabiini elfu ukailime kama ulotoka, ukikaa miaka saba jela basi una adhabu nyengine kwamba utakwenda utapewa miche yako ifike sabiini elfu.

Mhe. Mwenyekiti, hii nayo itawafanya wote ambao wanaofanya mambo ya ukorofi ukorofi katika karafuu watarudi nyuma. Jengine hii huyu ambaye amejaribu ameshiriki kala njama, safari hatotoka katika mtego huu kwa sababu huku nyuma alikuwa anatoroka hapati adhabu safari hii anapewa adhabu naiunga mkono mia juu ya mia. Mhe. Mwenyekiti, adhabu ya kifungu hichi naye atakwenda jela isipungue miaka mitano na isizidi miaka kumi lakini naye vilevile, atapata uchungu wa kulima miche ya mikarafuu elfu hamsini, ili na yeye aone uchungu wa kulima miche ya mikarafuu kwasababu anapokwenda kuigharibu mikarafuu akaichoma moto, akafanya magendo akainyima serikali kupata mapato basi aone nayeye dhiki ambayo inawapata wanaolima mikarafuu na serikali uchungu tuliokuwa nao wa kupata hasara hii ya mapato yetu.

Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma karafuu zilizokuwa zikikamatwa basi zinachukuliwa, zinapelekwa *ZSTC* zinauzwa halafu ziwe pesa anarudishiwa yule mhalifu sasa umeona wapi wewe mwizi halafu tena unakwenda kuuziwa mali yako unarudishia pesa ndio maana wakawa watu wengi, hii magendo ya karafuu mpaka mtu anajiita kama yeye ni doni yeye ndio rais kwa sababu waliokuwa wapewe adhabu. Kifungu hichi kinasema kama umekutwa na karafuu, karafuu zinataifishwa hupewi senti moja lakini vile vile, chombo chako kama umekwenda kusafirisha karafuu za magendo kwa gari, gari yako inakuwa mali ya serikali. Inataifishwa vilevile chombo chako kinataifishwa na vyombo vyengine kama gari nchikavu umekwenda kwa mfano kunako boti na kadhalika na kadhalika hata angani basi vyombo vyote hivi vitataifishwa.

Na maana ya kutaifishwa inakuwa nini vinapigwa mnada inakuwa mali ya taifa vinapigwa mnada vinauzwa, hili nalo ni pendekezo zuri sana Mhe. Mwenyekiti ambalo litawafanya hawa wanaoshirikia biashara hiyo ya magendo kuwarudisha nyuma na kupungua kasi zao, lakini nyengine Mhe. Mwenyekiti ambalo nalo tumeliona linafanyika kuna watu kunako vyombo, kuna tuhuma mbali mbali kwamba wafanyakazi wa *ZSTC*, au wafanyakazi KMKM au Polisi na kadhalika na kadhalika wanashirikia katika hujuma hizi za karafuu ama wanawasaidia kuwapa taarifa ama wanawasaidia kutorosha zile gari na zile karafuu kupitia vyombo vyao au wa- *escot* wale wahalifu, safari hii Mhe. Mwenyekiti sheria hii nawao watakwenda na maji. *(Makofi)*

Kwanza muhusika mwenyewe ofisa yule anayehusika Mhe. Mwenyekiti atachukuliwa hatua kifungu nam. 3 kinaeleza, vilevile kifungu chengine kinasema yule ambaye, chombo kinachofanya vile kama ni chombo, chombo hicho nacho kitapewa adhabu vilevile, kitachukuliwa hatua lakini pia yule atakayetoa siri kuhusu magendo haya akatoa siri mfano ni askari au KMKM au wafanyakazi wetu wa *ZSTC* ama watu wa kawaida masheha na wengine akatoa siri kwamba sasa hivi kuna jambo na akasaidia magendo ya karafuu na huyo pia naye atakuwa katika kosa la hatia na atapewa adhabu kali.

Hatahivyo, kuna operesheni Mhe. Mwenyekiti lakini yeye hausiki na operesheni ile au ukasema uongo maana yake kuna mambo yanafanyika katika magendo ya karafuu, watu wamegeuza viwanda sasa hivi karafuu inachukuliwa inachanganywa na magonyo inachanganywa na unga wa ngano, inachanganywa na sijui vitu vitu gani na mali na mafuta humo humo. Kwahivyo, lenyewe hili ni kosa lakini pia kusema uongo katika utaratibu mzima wa magendo, utaratibu mzima wa kufisadi karafuu nalo hilo Mhe. Mwenyekiti nalo ni kosa ambalo utapewa adhabu zake zimeelezwa kule mwanzo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana kwamba katika kifungu cha 27 kinasema kama taasisi kama yule Mkurugenzi nimeshasema pale mwanzo anachukuliwa hatua, Mhe. Mwenyekiti nimalizie kwa kusema kwamba ndugu zangu kipindi cha karafuu kinachokuja tutakuwa na kazi kubwa sana na tunatarajia Mwenyezi Mungu ametupa rehma kubwa kiasi, mwaka huu na hapo naomba baadhi ya wajumbe humu wana mikarafuu na wana uchungu na karafuu, na niwazoefu wa karafuu ningewaomba Mhe. Mwenyekiti wakaunga mkono kifungu hichi na wakarudi majumbani Unguja Kaskazini na Pemba kule kote kuwafahamisha wananchi dhamira yetu safari hii Mhe. Mwenyekiti ni kufanya Pemba ni sawa sawa na mpira ambao haungiliki, aliyekuwa ndani hatotoka na alokuwa nje ataingia kuleta karafuu. *(Makofi)*

Kwakweli, tumesema humu hatutaki karafuu kutoka nje ziingizwe na pia kuna hatia, ukileta karafuu kutoka nje tulipokea mwezi mwaka jana, magunia kama manne mpaka matano ya karafuu kutoka Tanga na Morogoro, najua nyote kama karafuu Zanzibar zina *brand* tumeshazim-*brand* na zina sifa yake na zinatambulika na bei yake ambayo imekubalika. Sasa kama kuna karafuu zinakuja nyengine zinaingia zinachanganyika na zetu matokeo yake tumepata kesi nyingi huko nyuma tukiambia karafuu Zanzibar zinaingia na matakata zinaingia na karafuu nyengine nyembamba, karafuu zetu sisi nzuri zimenyooka.

Kwahiyo, Mhe. Mwenyekiti hayo yatatusababishia kutuletea matatizo, tunachosema kwamba tunakubaliana kuchukua hatua hiyo...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri malizia muda.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Niseme tu naunga mkono mswada huu na nakuombeni ndugu zangu wote Waheshimiwa muunge mkono mswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Balozi. Sasa namwita Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aweze kutoa majibu na maelekezo, karibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti kwanza nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia Mswada wa Sheria hii. Waliochangia kwa jumla ni Waheshimiwa Wajumbe 9, nikianza na Mhe. Asha Abdalla Mussa ambaye amesoma taarifa ya Kamati ya Bajeti kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti, lakini pia Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Rashid Makame Shamsi, Mhe. Zulfa Mmaka Omar, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko

Hawa walitoa michango yao kwa kusema moja kwa moja, lakini kwa maandishi nina Wajumbe wanne (4)

1. Mhe. Shehe Hamad Matar,
2. Mhe. Simai Mohammed Said
3. Mhe. Masoud Abdrahman Masoud
4. Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Nawashukuru wote, niseme tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba mengi yaliyoulizwa tayari niliyatolea ufafanuzi wa kutosha wakati nikiwasilisha mpango wa maendeleo, lakini pia nikuwasilisha hotuba ya Bajet ya Serikali. Lakini na mengine mengi tuliyatolea ufafanuzi wakati tulipofanya semina yetu juzi na tulivyozungumzia masuala ya matumizi ya mashine ya *EFD*.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti walizungumzia sana kama iwapo tumezingatia mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2017. Niwaeleze tu kwamba tumezingatia kwasababu tulikuwa tuna mashirikiano mapema, wataalamu wa pande zetu mbili walikutana, kwahivyo marekebisho yaliyofanywa kwenye sheria ile tumeyazingatia katika sheria yetu ya fedha na katika ile Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ambayo itawasilishwa tukijaaliwa hapo kesho.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati walitaka kujua tutakapotumia hizi mashine za *EFD* na kwa bahati hatuna uhakika wa miundombinu ya umeme yaani utakapokatika. Kwakweli, niseme tu nchi nyingi za Afrika ambazo tayari zimeshaanza kutumia mashine hizi matatizo ya miundombinu ya umeme yapo lakini wanafanya, hicho siyo kikwazo cha kutoanza kutumia mashine. Hata wenzetu wa Tanzania Bara wanatumia mashine hizi na tatizo hilo huwa linatokezea. Lakini utaratibu upo na utaandaliwa kwa pale umeme utakapokatika basi ukaguzi utafanyika kutokana na kaguzi za kawaida zinazofanywa na watu wa ukaguzi wa bodi yetu ya mapato kwahivyo hakutokuwa na tatizo kubwa. Hata mashine ile isipofanya kazi bado unatakiwa utaratibu wa kutoa stakabadhi ya malipo kwa njia ya kawaida ifanyike. Kwahivyo, hilo sio tatizo lakini kama ninavyofanya teknolojia hii lazima na sisi tuingie kwa sababu ina manufaa makubwa sana katika ukusanyaji wa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la taaluma ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa wengi pamoja na Mhe. Simai Mohammed Said alilizungumza hili. Niseme kwamba ni muhimu sana taaluma hii itoke na itoke kwetu sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuifahamu vizuri lakini pia taaluma itoke kwa walipa kodi wenyewe ambao watakwenda kutumia teknolijia hii, lakini na hata walipa kodi wananchi wa kawaida na wao wajue. Kwahivyo, hiyo kazi itafanywa kwasababu bila ya mwananchi kudai risiti kazi bure. Kwakweli, kama hakudai risiti na

mfanyabiashara akaamua asitoe risiti kwa hivyo bado zitakuwepo bidhaa ambazo zinatoka bila ya kupatikana kwa risiti. Kwahivyo, ni muhimu na kuhamasisha wananchi kudai risiti kwasababu hayo makato wanayokatwa huko wanakatwa wao kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ni muhimu sana wajue kwamba serikali ina dhamira ya dhati na imekusudia na haitomdhulumu mtu yeyote kwasababu pia vyombo vya ulinzi vina haki ya kuwasimamisha watu wanapowaona na bidhaa kudai risiti. Wananchi na hili walijue kwasababu sasa tutaweka utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba wakikutwa na vitu wamechukua vyombo vya ulinzi vidai risiti na kama hana risiti na yeye atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria za nchi hii. Kwahivyo, hilo tutazidi kuelimishana na naamini wananchi wetu wasikivu wataweza ku-*comply* na sheria za nchi na kuweza kufanya kazi kwa utaratibu wa mfumo huu tunaouweka bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala alilizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma la mapato ya *visa* nimkubalie ni kweli kabisa tuliweka utaratibu wa kukusanya makusanyo yanayotokana na *visa* kupitia Benki ya *CRDB* na mapato yetu yaliongezeka kama alivyozungumza. Lakini hilo hata tulivyoamua kubalisha utaratibu wa leseni watu sasa walipe moja kwa moja nao yaliongezeka. Hayo ndiyo mageuzi tunayokusudia kuyafanya na serikali imeweka mkazo zaidi kuhakikisha kwamba sasa tunaingia katika mfumo wa ki-*electronic* kwanza hilo moja na mapato yanayotokana na mauzo ya *airtime* katika mashirika ya mawasiliano tayari tumeshawekea utaratibu huwo, utaratibu wambao unajulikana kama ni *Electronic Revenue Collection System* na tutajitahidi kadiri hali inavyokwenda kuingia katika teknolojia ya kisasa ya kuhakikisha kwamba makusanyo ya mapato yanakusanywa kwa ukamilifu wake.

Lakini kilichokusudiwa ndani ya mapendekezo ya Mswada wa Sheria hii ni kwamba malipo yanaweza kufanywa kwa kutumia simu ya mkononi na hii inafanywa kwa ajili ya kuwapunguzia wananchi usumbufu, kwa hivyo yale malipo madogo madogo wanaweza badala ya kwenda benki wanaweza wao wenyewe wakalipa kwa njia za kielekroniki lakini vile vile kwa kutumia simu za mkononi.

Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia kuhusiana na suala la nyumba bubu. Niseme nyumba hizi sisi tunajua kama zipo na wenzetu wa *ZRB* wanalifanyia kazi sana suala hili na lipo kwa mujibu wa sheria yetu ya usimamizi wa kodi (*Tax Administration Procedure Act*). Kwa utaratibu wa sheria hii nyumba za namna hii zote zinahitaji kusajiliwa, zisajiliwe halafu wanapewa viwango wambavyo wanastahiki kulipa. Viwango hivyo vinawekwa kwa mujibu wa nyumba ilipo, kama ipo katika maeneo ya kibiashara basi kiwango chake kinakuwa kikubwa zaidi na kama ipo katika mitaa ya makaazi nayo inakuwa na kiwango chake, lakini utaratibu upo.

Kama nilivyosema wakati nikifanya majumuisho jana katika Bajeti ya Serikali tulisema katika mwaka wa fedha 2017/18 tunakusudia kuuangalia mfumo mzima wa kodi nchini lakini pia kuviangalia vyanzo vyote vya kodi nchini na zile kasoro zilizokuwepo tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuzifanyia kazi.

Suala jengine lilizungumzwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi, alizungumzia kuhusiana na masuala ya uwezo wa Kamishna wa kutoa msamaha wa matumizi ya mashine za kielektroniki.

Niseme kwamba ni kweli lakini hilo limefanywa kwa makusudi kwa sababu katika utaratibu wa matumizi ya mashine hizi tutaanza kuzitumia kwa awamu. Kwahivyo, siyo wafanyabiashara wote kwa wakati mmoja wataanza kuzitumia mashine hizo. Kwa wale ambao watakuwa bado wanaendelea kutumia ule ule mfumo wa sasa wa kutoa stakbadhi za malipo kwa njia za kawaida bado kifungu hichi kinawapa fursa hiyo kwasababu Kamishna wa *ZRB* atakuwa ametoa msamaha kwa kipindi fulani kwa kundi hilo.

Lakini pia kuna walipa kodi wadogo wadogo ambao nao wanaweza kupewa msamaha maalum wa kuweza kutoa stakbadhi pamoja na ankara kwa njia za kawaida kwa sababu maalum. Kwa hivyo uwezo huwo nao anapewa kamishna, lakini uwezo huo pia utakuwepo ndani ya Kanuni ambazo zitatayarishwa zitakazoendana na utekelezaji wa sheria hiyo. Kwahivyo, asiwe na wasi wasi, lakini hata yule ambaye atatakiwa kutoa stakbadhi kwa njia ya kawaida utaratibu wake upo na kwa mujibu wa sheria hii ana asipofanya hivyo basi kwa mujibu wa kifungu cha 23(7) kimeweka adhabu ndani ya sheria hii ya kifungu cha 9 kifungu cha sheria mama 23(7) kimeweka utaratibu wa adhabu kwa huyu ambaye hatofuata masharti ya sheria hii.

Mhe. Rashid Makame Shamsi, pia alizungumzia suala la hii adhabu ya kupanda miche ya mikarafuu. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ameisema vizuri sana na sina haja ya kuitolea maelezo zaidi. Lakini niseme tu na mimi kwamba kwa kawaida Mahakama ikishakutoa hukumu yake basi kazi iliyobakia huwa ni kazi ya Chuo cha Mafunzo chenyewe. Zipo hukumu ambazo zinatoka kwamba mtu huyu amehukumiwa kifungo cha miaka mitatu na kazi ngumu. Sasa hakuna mtu wa nje tena anayekwenda kuamua kazi ngumu hiyo ni ipi lakini kazi ya Chuo cha Mafunzo ni kutekeleza hukumu iliyotolewa na Mahakama.

Kwahivyo, utaratibu wa jinsi ya kutekeleza hukumu hii utakuwa chini ya mikono ya Chuo cha Mafunzo wapi watakwenda kupanda mikarafuu hiyo wao wataweka utaratibu huo atakwenda kupanda katika misimu ipi na wakati gani ataweka utaratibu huo pia na kuweka idadi kamili mpaka ifikie kwa sababu ni sehemu ya adhabu iliyotolewa ma Mahkama kwa mujibu wa kosa alilolifanya.

Kuna mmoja alilizungumza na wale watakaoingiza karafuu na ikasemekana kwamba kwenye sheria kuna maelezo ya kwamba atakaingiza karafuu. Kwanza karafuu zitataifishwa lakini la pili atatakiwa alipe fedha zote mbili zinakwenda pamoja kwa thamani ya zile karafuu ambazo zimetaifishwa kwa hivyo kosa lake lote hilo atalitekeleza kwa pamoja.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar, alizungumzia suala la kitaaluma, nimeshalizungumza mashine za *EFD* lakini pia masuala ya risiti feki, na hii ya risiti feki pia Mhe. Masoud Abrahman Masoud aliizungumza na yeye alisema mpaka kuna hizi leseni za wenye maduka yale magamba yanayobandikwa pale yanakuwa wakati mwengine ni magamba feki, ni moja ya mambo ambayo sisi tutayafuatilia katiak mwaka wa fedha wa 2017/18 na wale wote tutakaowaona wanafanya kwa njia moja au nyengine kupoteza mapato ya serikali basi hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Naomba niseme jamani hili Waheshimiwa Wajumbe mtusaidie sana kwa sababu zinapochukuliwa hatua hawa tunaowachukuliwa hatua ni ndugu, jamaa, marafiki zetu wahisani zetu. Kwa hivyo tusije tukarudi hapa tukaanza kuwatetea hawa hawa kwa sababu hatua kali tutazichukua kwa mtu yeyote ambaye atakwenda kinyume na matakwa ya sheria hizi na anafanya kujaribu kukwepa ulipaji wa kodi stahiki zilizowekwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo tukichukua hatua sote tusimame kwa pamoja kwa sababu njia hiyo ndiyo itakayotusaidia kuendeiendeleza mbele nchi yetu na jamii kupata unafuu badala ya kuwatetea watu wachache ambao wanajilimbikizia mami ilisiyohalali. Maana hujakatazwa kujilimbikizia mali lakini isivyo halali kwa faida zao lakini huku wakinyima fursa wananchi walio wengi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa alizungumzia kwamba uwanzishaji wa huu mfumo wa kielektroniki ambao utaanzishwa na kamishna je, pia utaanzishwa katika serikali za mitaa. Nilisema mwanzo kwamba tunakwenda awamu kwa awamu Awamu ya kwanza tutaweka mahsusi itatumika kwa baadhi ya taasisi za serikali lakini vilevile kwa baadhi ya wafanyabiashara na walipa kodi. Lakini pia tutakuwa taratibu tunaendelea kwa wafanyabiashara na walipa kodi wengine.

Vilevile, niseme kwamba utaratibu wetu wa kodi kuna mfumo ambao una *level* tatu kuna Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo mifumo ipo baadhi yake inaandaliwa na kama nilisema kuna mfumo ambao sasa hivi umeshaandaliwa uliwashirikisha *ZRB* na *TRA* mfumo ambao ni wa kieletroniki unaoweza kukata fedha katika makampuni ya simu, makampuni ya mawasiliano moja kwa moja na kuingiza katika *account* ya ZRB na *TRA* sasa mfumo huu mbali.

Lakini pia kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika *level* nyengine ya ukusanyaji wa mapato nao tunaanzisha mfumo huu wa kutumia mashine ya kielektroniki. Wenzetu wa Serikali za Mitaa tayari wameshaanza na wao utaratibu na wameshaanza mazungumzo pia ya kuona wanaweza kuweka utaratibu gani na mfumo gamo gani wa kukusanya kodi katika *level* hiyo ya Serikali za Mitaa. Kwahivyo, yote yafanyika kwa wakati mmoja na tunatarajia kadri hali itakavyoendelea basi itakuwa tumefikia hatua nzuri sana ya kukusanya mapato ya serikali.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nimeyazungumza kwa ujumla kwa sababu na Waheshimiwa Wajumbe waliochangia walihangia kwa ujumla wake, lakini nirudie kusema kwamba Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko amenisaidia sana hasa katika suala zima la mabadiliko ya Sheria Inayohusika na Magendo ya Karafuu, ametoa ufafanuzi mzuri na sina haja ya kuurudia ufafanuzi uliokwisha kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naomba kutowa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha hoja imetolewa. Sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wale wanaounga mkono hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja imetowa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2017

Sehemu ya Kwanza

Jina Fupi na Kuanza Kutumika

Kifungu 1 Jina Fupi na kuanza kutumika

Sehemu ya Pili

Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya 2009

Kifungu 2 Kusomwa
Kifungu 3 Marekebisho ya Kifungu cha 3 Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 4 Marekebisho ya Kifungu cha 4
Kifungu 5 Marekebisho ya Kifungu cha 7 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 6 Marekebisho ya Kifungu cha 21
Kifungu 7 Marekebisho ya Kifungu cha 22
Kifungu 8 Kuongeza Kifungu Kipya cha 22(a) Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 9 Marekebisho ya Kifungu cha 23 Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 10 Marekebisho ya Kifungu cha 24 Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 11 Marekebisho ya Kifungu cha 31(a) Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 12 Marekebisho ya Kifungu cha 43
Kifungu 13 Marekebisho ya Kifungu cha 51
Kifungu 14 Kuongeza Kifungu Kipya ya 52(a) Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 15 Kuongeza Kifungu Kipya cha 53(b) Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Tatu

Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya 1998

Kifungu 16 Kusomwa Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 17 Marekebisho ya Kifungu cha 2 Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 18 Marekebisho ya Kifungu cha 5 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 19 Marekebisho ya kifungu cha 6 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20 Marekebisho ya kifungu cha 16

Sehemu ya Nne

Marekebisho ya Sheria ya Kodi za Mafuta namba 7 ya mwaka 2001

Kifungu 21 Kusomwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 22 Marekebisho ya kifungu cha 2
Kifungu 23 Marekebisho ya kifungu cha 3

Sehemu ya Tano

Marekebisho ya Sheria ya Maendeleo ya Karafuu namba 2 ya mwaka 2014

Kifungu 24 Kusomwa
Kifungu 25 Markebisho ya kifungu cha 3
Kifungu 26 Marekebisho ya kifungu cha 19
Kifungu 27 Kuongeza vifungu vipya vya 19(a), 19(b) na 19(c)
Kifungu 28 Kuongeza vifungu vipya vya 26(a) na 26(b) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 29 Marekebisho ya kifungu cha 27
Kifungu 30 Marekebisho ya kifungu cha 29

Sehemu ya Sita

Marekebisho ya Ajira namba 11 ya 2005 pamoja na Marekebisho yake

Kifungu 31 Kusomwa
Kifungu 32 Marekebisho ya kifungu cha 100 pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Saba

Marekebisho ya Sheria ya Mafunzo ya Amali namba 8 ya mwaka 2006

Kifungu 33 *Construction* pamoja na marekebisho yake
Kifungu 34 Marekebisho ya kifungu cha *Amendment of Section 27* pamoja na marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu nakukubali bila ya marekebisho. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaounga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wanyanyuwe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja imetowa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2017

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutowa hoja kwa Mswada wa Sheria ya Fedha, maana Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2017 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wale waounga mkono hoja ya Mhe. Waziri, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa
mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, ahsanteni sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuweza kufanya shughuli zetu hizi za leo hadi hapa ikawa tumefikia mwisho kwa uzuri na kwa utulivu kabisa. Nampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na wajumbe ambao wamechangia miswada mbalimbali iliyowasilishwa mbele yetu. Kwahivyo, nachukua fursa hii kuliakhirisha Baraza hili hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 21/06/2017 saa 3:00 asubuhi)